SUPA JACKPOT
TZS. 1,062,078,169
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 4 &8

**MBWA MWITU;** bidhaa ipatikanayo Afrika tu, hatarini kutoweka




UKURASA 13

Nipashe
Jumamosi Desemba 31, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581176
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# DC kulipa mil 80/- kwa udhalilishaji



UKURASA 2



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizungumza na watumishi wa Ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini, jijini Pretoria. Kulia ni Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, na wa pili kulia ni Kaimu Balozi wa Tanzani nchini humo, Peter Shija. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# CHADEMA yazidi kulia Katiba Mpya, Tume huru ya Uchaguzi

UKURASA 3

# Mshtakiwa dawa kulevya adaiwa kufia mahabusu

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA SC, YANGA DIMBANI APRILI 9 UK. 32
**KATUNI** UK. 6

# Mtuhumiwa wa dawa za kulevya adaiwa kufariki dunia mahabusu

**Na Grace Gurisha**

WAKILI wa utetezi katika kesi ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin kilo 20, Hassan Yassin, ameieleza Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kuwa mteja wake, Henry Ozoemena, raia wa Nigeria, amefariki dunia wiki mbili zilizopita katika mahabusu ya Gereza la Segerea.

Mbali na Ozoemena, washitakiwa wengine katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi ni raia wa Latvia, Linda Mazure na Martins Plavins, ambao ni mtu na mpenzi wake. Wanatuhumiwa kutenda kosa hilo Aprili 19, 2019.

Yasini alitoa taarifa hiyo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rhoda Ngimilanga, wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa na Wakili wa Serikali, Faraja Ngukah.

Alidai kuwa mshitakiwa wa pili katika kesi hiyo Ozoemena amefariki dunia katika mahabusu ya Segerea baada ya kupata tatizo la shambulio la moyo.

Aliendelea kudai kuwa mteja wake alifariki dunia wiki mbili zilizopita na tayari mwili wake umesafirishwa kwenda nchini kwao, Nigeria kwa ajili ya taratibu za mazishi.

Pia aliiomba mahakama kuamuru upande wa mashitaka kukamilisha mapema usajili wa nyaraka muhimu Mahakama Kuu, ili kesi hiyo iendelee kwa hatua nyingine kwa sababu ni ya muda mrefu.

Baada ya Wakili Yasini kudai hayo, aliiomba mahakama iwaelekeze upande wa mashitaka uwasilishe taarifa hiyo muhimu ili kesi hiyo iendelee kwa hatua nyingine.

Hakimu Ngimilanga baada ya kusikiliza maelezo ya pande zote, aliuagiza upande wa mashtaka ujitahidi kukamilisha mapema nyaraka hizo.

Kesi hiyo iliaharishwa hadi Januari 13, mwakani itakapotajwa na washtakiwa wamerudishwa rumande kwa sababu shtaka wanalokabiliwa nalo halina dhamana.

Katika hati ya mashtaka, Mazure anadaiwa kutenda kosa hilo Aprili 17, 2019 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Dar es Salaam kwa kukutwa na kilo 20 za Heroin zikiwa katika mabegi mawili.

Inadaiwa kuwa Aprili 19, 2019 mshitakiwa Plavins alikamatwa eneo la Kariakoo, Dar es Salaam, na alipohojiwa alidai kumsafirisha Linda kutoka Latvia kuja Tanzania kuchukua dawa hizo.

Pia Aprili 19, 2019 mshtakiwa Ozoemena alikamatwa na katika mahojiano na Jeshi la Polisi, alikiri kumpatia Linda begi moja lililokuwa na dawa za kulevya aina ya Heroin zenye uzito wa kilo 15.



Wananchi kata ya Moa wilayani Mkinga mkoani Tanga na vijiji jirani wakiwa wamekusanyika katika jengo la soko la Samaki lililopo kando ya Bahari kwa ajili ya kuwapokea majeruhi ambao walikuwa wakiokolewa majini na Vikosi vya Ulinzi na Usalama baada ya boti waliyokuwa wakiitumia kuzama, Wavuvi 19 waliokolewa na mmoja alifariki dunia jana alfajiri. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# DC kulipa mil. 80/- udhalilishaji

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Tabora, imemhukumu aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Erick Kitwala, kumlipa, Alexunder Ntonge Sh. Milioni 80 kwa kumdhalilisha mbele ya familia yake.

Akitoa hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Jovith Kato, alisema ametoa hukumu hiyo baada ya kusikiliza pande zote mbili na pamoja na ushahidi uliotolewa mahakamani hapo.

Komanya ambaye uteuzi wake ulitenguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Juni, mwaka huu, alikuwa akikabiliwa na kesi ya madai ya fidia ya Sh. milioni 140 kutokana na vitendo vya udhalilishaji alivyomfanyia Ntonge.

Katika shauri hilo la madai namba 4 la mwaka 2022, mdai alitaka alipwe Sh. milioni 80 kutokana na kuzuiwa uhuru wake, Sh. milioni 30 kutokana na tendo la kukamatwa na kushtakiwa kwa nia ovu na Sh. milioni 30 kwa kudhalilishwa utu wake.

Ntonge kupitia kwa wakili wake, Kelvin Kayaga, alidai kuwa siku hiyo, Komanya akiwa Mkuu wa Wilaya ya Tabora akiwa ameambatana na askari polisi, walifika nyumbani kwa mdai eneo la Ipuli na kumkamata na kisha kumdhalilisha.

Aliongeza kuwa Komamya akiwa na askari polisi wawili wenye bunduki aina ya SMG, baada ya kumkamata walimdhalilisha mbele ya familia yake na majirani zake ikiwa ni pamoja na kumwamuru apige magoti barabarani.

Mahakama hiyo ilifikia hatua hiyo baada ya kumaliza kusikiliza mashahidi wa pande zote mbili ukiwamo wa Mkuu wa Polisi Wilaya ya Tabora, George Wilbard, ambaye aliitwa kama shahidi wa mdaiwa, Kitwala Komanya.

Katika utetezi wake mbele ya Hakimu Katto huku akiongozwa na wakili wa kujitegemea, Issa Mavulla, Komanya alidai kuwa amefunguliwa shauri hilo kwa nia ya kumkomoa na kumkomesha.

Katto alikuwa Hakimu wa tatu kusikiliza shauri hilo ambalo awali lilianza kusikilizwa na Hakimu Sigwa Nzige, lakini mdaiwa alimkataa na kubadilishiwa mwingine.

Komanya alikana kuhusika na tuhuma zinazomkabili za vitendo vya udhalilishaji dhidi ya Ntonge wakati wa uongozi wake akiwa Mkuu wa Wilaya ya Tabora.

Hata hivyo, alikiri kuambatana na Wilbard kwenda nyumbani kwa Ntonge kwa ajili ya kumkamata akituhumiwa kutumia mitandao ya kijamii kumdhalilisha.

# Serikali yasema hakuna uhamisho wanafunzi wa kutwa kwenda bweni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Prof. Riziki Shemdoe, amesema hakutakuwa na uhamisho wa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwenye shule za kutwa kwenda bweni.

Prof. Shemdoe alitoa msimamo huo wa serikali juzi jijini hapa katika kikao kazi cha kufanya tathmini ya usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini kwa mwaka 2022 kwa maofisa elimu wa mikoa.

Alisema, tangu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Angellah Kairuki, atoe taarifa ya kuwapangia shule wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2023 Desemba 14, mwaka huu, ofisi yake imekuwa ikipokea maombi kutoka kwa wazazi au walezi watoto wao kuhamia kwenye shule za bweni kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za ugonjwa au matamanio ya wazazi na watoto.

Kutokana na hali hiyo, Prof. Shemdoe alisema hakutakuwa na uhamisho wa wanafunzi waliochaguliwa shule za kutwa kwenda kwenye shule za bweni kwa kuwa upangaji wa wanafunzi umefuata vigezo na taratibu zilizowekwa.

"Ofisi ya R ais -TAMISEMI inasisitiza kuwa hakuna uhamisho kutoka shule ya kutwa kwenda bweni kwa sababu wale waliopangiwa bweni wamekidhi vigezo vya kuchaguliwa katika shule hizo."

"Kwa wanafunzi wenye changamoto za kimazingira, mfano amehama makazi ya awali, wawasilishe changamoto hizo kwa makatibu tawala wa mkoa ili zitatuliwe maana upangaji wa wanafunzi kwenye shule umezingatia ukaribu wa shule na makazi ya wanafunzi. Endapo wamehama makazi ya awali, kunaweza kutokea changamoto ya umbali," alisema.

Prof. Shemdoe alisema kupangiwa shule kwa wanafunzi kumezingatia viwango vya ufaulu, ushindani pamoja ukaribu wa shule na makazi.

Aidha, idadi ya wanafunzi waliopangiwa kwenye shule za bweni imezingatia viwango vya juu vya ufaulu na nafasi zilizokuwapo katika shule hizo ili kuepusha msongamano kwa wanafunzi darasani na mahali pa kulala.

"Endapo zitatokea nafasi za bweni zitakazohitajika kujazwa hapo baadaye, maombi yatakayokuwa yamefikishwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI makao makuu, yatachambuliwa na kamati maalum ambayo itaangalia sifa za waliomba kuhamishiwa huko," alisisitiza.

Pia alitoa wito kwa wazazi kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa wanaripoti shuleni kwa wakati na kwamba hakutakua na chaguo la pili la mwanafunzi.

"Kwa mwaka huu hakutakuwa na chaguo la pili la wanafunzi kwa sababu fedha zilizotolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika sekta ya elimu zimetosha kuboresha miundombinu ya kuwachukua watoto wetu wote kwa mkupuo mmoja."

"Tangu Rais aingie madarakani ameshatoa fedha zilizowezesha kujenga zaidi ya vyumba vya madarasa 20,000 ndani ya miaka miwili, hatua ambayo imewaondolea adha watoto kwa kuanza masomo kwa pamoja huku wazazi wakiwa hawajachangishwa kitu," alisema.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Dk. Selemani Jafo akizindua mradi wa kisima cha maji katika kijiji cha Nghambi wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma wakati wa ziara ya kukagua na kuzindua miradi inayotekelezwa kupitia Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR) katika Halmashauri ya Mpwapwa mkoani Dodoma jana.**PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# CHADEMA yazidi kulia Katiba mpya, tume huru

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KATIBU Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA, John Mnyika, amesema wataendelea kudai Katiba mpya na tume huru na haki ya uchaguzi kuelekea katika uchaguzi mkuu 2025.

Akitoa msimamo huo, amesema wataendelea kupambana kupata Katiba Mpya kwa amani ili kuhakikisha inapatikana kabla ya uchaguzi mkuu.

Mnyika alibainisha hayo juzi katika mkutano mkuu maalumu wa chama hicho mkoani Mwanza. Pamoja na mambo mengine, alisema chama hicho kitaendelea kuwatetea wanyonge bila kuiweka pembeni ajenda ya katiba mpya.

Alisema watahakikisha mchakato wa mabadiliko ya katiba mpya unapelekwa katika kikao cha Bunge cha Februari, mwakani, ili kuhakikisha wanafanya marekebisho ya Katiba kabla ya Bunge la Septemba 2023 watakapokuwa tayari wamechelewa kufanya mchakato huo kwa kuwa utakuwa umeanza utaratibu wa uchaguzi mkuu.

Mnyika pia aliwataka wanachama kuhakikisha wanakuwa na umoja katika kupigania Katiba mpya pamoja na tume huru na haki ya uchaguzi ili kuwawezesha kuingia katika uchaguzi mkuu wakiwa tayari wana Katiba mpya.

Kuhusu umiliki wa ardhi, Mnyika alisema sheria za umiliki wa ardhi bado ni kandamizi, hivyo watahakikisha wanalihusisha katika Katiba mpya ili kumwezesha mwananchi kuwa na umiliki wa ardhi na vitu vyote vilivyomo ndani yake.

Alisema hatua hiyo itasaidia kupunguza na kumaliza kabisa migogoro ya ardhi ikiwa ni pamoja na kutoa haki ya hatimiliki kwa wakazi waishio milimani katika jiji la Mwanza kutokana na mpango wa mabadiliko ya jiji jipya la Mwanza.

Kuhusu mikutano ya hadhara, Mnyika alisema chama hicho kitaanza rasmi mikutano yake ifikapo 2023 bila kujali zuio lolote la serikali kwa kuwa hatua hiyo ni ya haki, kisheria na kikatiba.

Akieleza msimamo wa chama hicho katika uchaguzi mkuu, Mnyika alisema CHADEMA itaendelea kujipanga na kujiandaa na uchaguzi mkuu huku wakiendelea kuomba haki yao ya kupata katiba mpya.

Aidha Mnyika aliwataka wanachama wa chama hicho waliojisajili kidigitali kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika uchaguzi wa ndani unaotarajiwa kufanyika hivi karibuni na kuwataka kuendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za chama na kujiepusha na mpasuko wa kichama katika kipindi cha utiaji nia.

John Heche, mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, licha ya kuwahimiza wanachama wa chama hicho kuhakikisha wanakuwa na nguvu moja katika kutetea haki, aliishukuru serikali kuendelea kufuata utaratibu katika kuwalipa fidia za ardhi wananchi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa wakiwamo wa mkoa wa Mara.

Akizungumza katika mkutano huo, Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Chadema (BAVICHA), John Pambalu, aliwahimiza wananchi waishio milimani kuhakikisha wanapigania upatikanaji wa hati za viwanja na si leseni kama walivyopatiwa na halmashauri ya jiji.

Pambalu alisema hatua hiyo itawasaidia katika kuthaminisha ardhi yao pindi mpango wa kubadili maeneo ya milima na kujengwa maghorofa kuanzia nne ukiwa ni mpango maalumu wa kuboresha jiji la Mwanza.

Aidha, aliomba serikali kujali maslahi ya wafanyabiashara wadogo wadogo, maarufu kama machinga, kwa kuwapangia maeneo yanayofaa kufanyia biashara tufauti na yale waliyopatiwa yenye ubovu wa miundombinu na kujaa maji kila mara na kuharibu mitaji ya wafanyabiashara hao.

Sylvester Masinde, Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini CHADEMA, alisema katika kuhakikisha wanatetea haki za wananchi, wataendelea kupaza sauti kuomba kupata Katiba mpya na si tume huru ya uchaguzi ambayo pia inatokana na Katiba iliyopo ambayo haikidhi matakwa ya Muungano na uchaguzi huru na haki.

Mkutano huo uliwakutanisha wanachama wa chama hicho pamoja na viongozi kutoka Kanda ya Ziwa Victoria na mgeni rasmi alikuwa Mnyika aliyeambatana na Mwenyekiti wa BAVICHA.

# Wauguzi wadaiwa kusababisha kifo cha kichanga

**Na Jumbe Ismailly,**
SINGIDA

BAADHI ya wauguzi wa Kituo cha Afya cha Sokoine, Manispaa ya Singida waliokuwa zamu kwenye wodi ya wazazi, wamedaiwa kusababisha kifo cha kitoto kichanga cha siku moja.

Madai hayo yametolewa na Mwajuma Mohammed, Mkazi wa Mtaa wa NHC mjini hapa huku akisema wahudumu hao wamesababisha kifo cha mtoto wa binti yake aliyekwenda kujifungua katika kituo hicho.

Mwajuma ambaye ni mama mzazi wa Halima, alisema Desemba 24, mwaka huu, majira ya takribani saa 6:00 usiku, binti yake huyo aliyekuwa na ujauzito wa kwanza, alianza kusumbuliwa na uchungu wa uzazi na ndipo walipompeleka katika kituo hicho kwa ajili ya huduma.

Alisema baada ya kufika na kupokewa, mgonjwa wake alipimwa na kisha kupatiwa kitanda cha kupumzika na kwamba asubuhi ya Desemba 25, wauguzi wa zamu waliwaamuru kutoka nje ya wodi aliyokuwa amelazwa ili wafanye usafi.

Kwa mujibu wa Mwajuma (50), wakati yeye akiwa nje ndipo binti yake alizidiwa na uchungu lakini alipoomba kuingia ndani ili akamsaidie, hakuruhusiwa.

Pamoja na kutokuruhusu, alisema wauguzi hao walizidi kumtia uchungu kwa maneno ya kifedhuli kwamba endapo mwanawe anataka kujisaidia haja kubwa na ajisaidie tu hapo hapo alipokuwa amelala.

"Niliienda kwa nesi kumpa taarifa za kuzidiwa kwa binti yangu ili niweze kwenda kumsaidia haraka lakini nesi huyo alinijibu kwamba baada ya kumpima binti yake imeonekana atajifungua saa sita usiku, hivyo asiwapigie kelele," alidai mama huyo.

Aidha, Mwajuma ambaye ni mjane, alisema wakati akipokea majibu kutoka kwa wauguzi hao, ndipo kwa msaada wake mwanawe huyo alijifungua pale pale kwenye kitanda alichopumzishwa kusubiri kuingizwa kwenye chumba cha kujifungulia.

Alisema baada ya wauguzi hao kuona hali ya mama huyo kutoa huduma asiyostahili kuifanya kituoni hapo, ndipo alitakiwa atoke nje kwa madai kwamba wanataka kumsafisha. Kutokana na hali aliyokuwa nayo kichanga huyo, waliondoka kwenda katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mandewa ambako alipokewa na kuanza kupatiwa huduma.

Hata hivyo, mama huyo alisema ilipofika jioni ya Desemba 26, kichanga hicho kilizidiwa na kupoteza maisha na baada ya tukio hilo, waliruhusiwa majira ya saa 1:00 kurudi nyumbani.

"Hili ni tukio la pili kutokea kwenye familia yangu kwani mwaka 2020 nilimpeleka msichana wangu mwingine (siyo huyu) kwenda kujifungua Kituo cha Sokoine lakini sikuridhishwa na huduma zinazotolewa na baadhi ya wauguzi kwani walikuwa wakiwasumbua sana wagonjwa wanaokwenda kujifungulia kituoni hapo.' Alisema.

Halima Mohamedi (18) ambaye ulikuwa ujauzito wake wa kwanza, alikiri kupatwa na masahibu hayo kwa kuwa licha ya kutoa taarifa kwa wauguzi hao, aliambiwa kuwa anasumbua wauguzi, hivyo awaache wafanye kazi zao kitaalamu.

Husseini Njiku, Mwenyekiti wa Mtaa wa NHC, alipoulizwa juu ya suala hilo, alikiri kuwa Desemba 26, kulikuwa na msiba wa kijukuu cha Halima, kifo kinachodaiwa kusababishwa na wauguzi wa Kituo cha Afya Sokoine.

Alisema kabla ya mazishi ya kichanga hicho wauguzi wawili kutoka katika Kituo hicho walifika na kuandika maelezo ya mfiwa, walishiriki mazishi na kisha kuondoka.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Kulanga Kanyanga, alikiri kuwapo kwa tukio hilo na kwamba tayari timu imeundwa kuchunguza tukio hilo ili kupata ukweli.

"Ni kweli tukio hilo tumelipata na mpaka sasa hatua zimeanza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwaandikia barua wauguzi waliokuwa zamu ili watoe maelezo. Timu ya kuchunguza tukio hilo imeshaundwa na kuanza kazi na ikibainika walihusika, hatua dhidi ya wahusika zitachukuliwa," alisema.

RIPOTI MAALUM

# Mbwa mwitu; bidhaa ipatikanayo Afrika pekee, hatarini kutoweka

Na Sanula Athanas

## Tatizo? Wakazi jirani, utata kwenye shoroba...

NI majira ya alasiri, kundi la ndege wa aina mbalimbali linaonekana likila mzoga wa mnyama kwenye Hifadhi ya Taifa Serengeti (SENAPA). Kwa wenye uzoefu na mandhari ya hifadhini, mizoga ya aina hiyo hugombaniwa na fisi na mbwa mwitu.

Kinachoshuhudiwa hifadhini Serengeti - mzoga wa mnyama unaliwa na ndege pasi na kuwapo mbwa mwitu, mara moja kinaikumbusha Nipashe kwamba lipo tatizo la kupungua idadi ya mbwa mwitu kwenye maeneo ya hifadhi nchini, hata kuonesha ishara hatari ya kutoweka kwao.

Kwa mujibu wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), hadi Desemba 2020, yaani miaka miwili iliyopita, Mfumo wa Ikolojia ya Serengeti (Serengeti Ecosystem) ulikuwa na mbwa mwitu 220 sawa na asilimia 3.33 ya mbwa mwitu wote 6,600 wanaokadiriwa kuwapo duniani kwa sasa.

Mfumo wa Ikolojia Serengeti unajumuisha SENAPA, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na Hifadhi ya Masai Mara ya nchi jirani ya Kenya.

Albert Mangowi, Mhifadhi - Sayansi ya Uhifadhi katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi, anakiri kupungua kwa mbwa mwitu kwenye maeneo mbalimbali ya hifadhi nchini kutokana na sababu mbalimbali, zikiwamo uingilii na na kuuliwa na wafugaji.

"Awali mbwa mwitu walikuwapo kwenye hifadhi karibu zote nchini lakini kwa sasa wamebaki kwenye maeneo machache.

"Sasa unaweza kuwapata mbwa mwitu katika Mfumo wa Ikolojia wa Serengeti - Masai Mara, Mfumo wa Kiikolojia wa Mkomazi - Savo, Mfumo wa Kiikolojia wa Ruaha - Katavi, Mfumo wa Kiikolojia wa Ugalla, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na Pori la Akiba Selous," anabainisha.

Hata hivyo, mhifadhi huyo hayuko tayari kutaja idadi kamili ya mbwa mwitu waliopo kwenye hifadhi hizo, akiwa na hoja kwamba suala hilo ni nyeti. Tanzania ina hifadhi za taifa 22.

### TISHIO KUTOWEKA

Mhifadhi Mangowi anafafanua kiini cha kupungua kwa mbwa mwitu ni pamoja na tabia yao ya kutembea kwa makundi wakitafuta kitoweo hadi kwenye maboma ya ng'ombe, hivyo baadhi ya wafugaji huwapa sumu ili kuwadhibiti.




"Sababu nyingine ni mlipuko wa magonjwa kama vile kichaa cha mbwa. Pia pale wanapovamia mifugo ya jamii ya wafugaji inayoishi pembezoni mwa hifadhi, huuliwa kutokana na migongano hiyo kati yao na wafugaji," anafafanua.

Ni hoja inayoungwa mkono na Mratibu wa Faru kitaifa, Philbert Ngoti anayebainisha kuwa mbwa mwitu na faru ni wanyama walio katika hatari ya kutoweka, akiwa na ufafanuzi zaidi, akitamka:

"Mbwa mwitu wanapungua kwa sababu makazi yao yanachukuliwa na binadamu. Kingine ni muingiliano na binadamu. Unakuta wanakula ng'ombe na wananchi wanaamua kuwaua. Sababu nyingine ni magonjwa.

"Mbwa mwitu anatembea kilometa 75 kila siku, hawatulii sehemu moja, hivyo wakati mwingine wanayafikia makazi ya watu. Mbwa mwitu wengine wanakwenda hadi nchi jirani na hawarudi tena.

"Mikakati inayofanyika ni kuwakamata na kuwahifadhi kwa kuwafuga, wakishazaliana tunakwenda kuwaachilia kwenye hifadhi.

"Hivyo, tunatoa wito kwa wananchi waache kuwaua mbwa mwitu kwani wamekuwa wakipewa sumu," Ngoti anasema na kubainisha kuwa hadi Desemba 2020, Mfumo wa Ikolojia wa Serengeti (Serengeti Ecosystem) ulikuwa na mbwa mwitu 220 tu.

Constantine Kanyasu, mdau wa utalii na uhifadhi ambaye pia ni Mbunge wa Geita Mjini, ananyoshea kidole uvamizi wa shoroba za wanyamapori na hujuma zinazofanywa na wenyeji wa maeneo yanayopakana na hifadhi, kuwa mzizi wa kupungua kwa idadi ya mbwa mwitu nchini.

Kanyasu aliyekuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii wakati wa uongozi wa Rais John Magufuli (Hayati), anawasilisha uzoefu wake, akisema: "Mtu anapoamua kuweka sumu kwenye mzoga, anaua mbwa mwitu wengi kwa wakati mmoja, maana hawa (mbwa mwitu) wanatembea wakiwa kwenye kundi kubwa.

"Kuna maeneo shoroba zimevamiwa na shughuli za kibinadamu, ule ushoroba wa KINAPA hadi Hifadhi ya Taifa Arusha umezibwa na shughuli za binadamu. Maeneo yale mbwa mwitu wametoweka kabisa.

"Kwa hiyo, rai yangu katika hili, elimu itolewe kwa jamii inayoishi karibu na hifadhi isiwaue kwa kuwashambulia au kuwategea mizoga yenye sumu maana mbwa mwitu ni wanyamapori muhimu sana hifadhini. Hawa ndiyo wafanya usafi wa hifadhi, wanakula mizoga na kuzifanya hifadhi zetu kuwa safi."

### MIKAKATI TANAPA

Inaporejewa mikakati ya kitaifa kukabiliana na tishio la kutoweka kwa mbwa mwitu, Mhifadhi Mangowi anasema: "Utafiti uliofanyika kwenye maeneo mbalimbali, unaonesha wanyamapori hao wako hatarini kutoweka.

"Hivyo, tumeanza kuwazalisha ili kuwarejesha kwenye maeneo yao. Takwimu upo uwezekano wa kuongezeka kwa idadi yao kupitia jitihada hizi ingawa bado kuna migongano baina yao na jamii za wafugaji wanaochunga pembezoni mwa hifadhi zetu.

"Katika jitihada za kuwahifadhi mbwa mwitu ili wasitoweke kwenye maeneo yao ya asili, serikali imeanzisha Mradi wa Kutunza na Kuzalisha Mbwa Mwitu katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi.

"Mradi huu upo tangu mwaka 2000 ukiwa na lengo la kuzalisha mbwa mwitu na baadaye kuwapeleka wanyamapori hao kwenye maeneo yao ya asili ndani ya Mfumo wa Ikolojia wa Mkomazi-Savo na kwenye maeneo mengine yaliyowahi kuwa na mbwa mwitu ili kuwarudisha katika maeneo yao ya asili.

"Sambamba na hili, serikali imeanzisha programu ya ufuatiliaji wa mbwa mwitu kwenye maeneo yanayozunguka Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, ikisimamiwa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI) kwa ajili ya kuhakikisha usalama na uhifadhi wa mbwa mwitu walio ndani na nje ya hifadhi kulingana na mazingira yao ya asili, ili kuinusuru hii idadi ndogo ya mbwa mwitu iliyobaki."

### HATARI KIUCHUMI

Tishio la kutoweka kwa wanyamapori hao wanaosifika kwa kufanya usafi (kula mizoga) hifadhini, kunaiweka njiapanda Sekta ya Utalii, pia ajira za maelfu na uchumi wa nchi.

Kwa mujibu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Sekta ya Utalii inaingiza robo (asilimia 25) ya fedha za kigeni nchini na kuchangia asilimia 17.5 ya Pato la Taifa huku ikiwa ni mwajiri wa Watanzania 600,000 ofisini na wadau wenzao takribani milioni mbili inayowapa ajira zisizo za moja kwa moja.

### TABIA ZAO

Mtaalamu wa Wanyamapori, Sadick Omary anawataja mbwa mwitu ni wanyama jamii ya mbwa wenye sifa za kuwa na umoja na ushirikiano mkubwa wanapokuwa kwenye mawindo.

Anasema wana manyoya yenye aina mbalimbali za rangi zenye kuvutia zikiwamo nyekundu, nyeusi, nyeupe, kahawia na njano, kila mmoja ana mpangilio wa rangi mwilini mwake ambao mbwa mwitu mwingine hawezi kuwa nao.

"Rangi za manyoya yao huwasaidia kujificha kwenye mazingira wanayoishi na hivyo kuwa vigumu kuonekana kwa maadui au wanyama hatarishi kwao.

ITAENDELEA Uk. 8

# Bil. 7.11/- kuunganisha umeme mkoani Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA) umepanga kutumia Sh. bilioni 7.11 kwa ajili ya kusambaza umeme awamu ya tatu katika vijiji vilivyoko pembezoni mwa Halmashauri ya Manispaa ya Singida ambavyo havijapata nishati hiyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Mipango na Utafiti wa REA, Nicolaus Moshi, alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa mradi mpya wa awamu ya tatu wa kusambaza umeme vijijini uliofanyika katika kitongoji cha Kitope Darajani Kata ya Mwankoko utakaotekelezwa kwenye vitongoji 34 vilivyoko katika kata tisa.

Alisema katika mradi huo ambao unatarajiwa kuwanufaisha zaidi ya wananchi 2,000 kutajengwa kilometa 40.5 za msongo wa kati na msongo mdogo na utakamilika mwaka 2024.

Moshi alisema mkandarasi wa mradi huo, Central Electrical International Limited kutoka Dar es Salaam ndiye aliyepewa zabuni kusambaza umeme kwa mkoa wa Singida na amewataka wananchi kutumia fursa ya mradi huo kuunganishiwa huduma ya umeme.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Singida ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskasi Muragili, alisema vijiji vingi vilivyokuwa pembezoni mwa miji vilikuwa vinaonekena vimetengwa kutokana na kukosa huduma muhimu za kijamii kama vile umeme maji, afya na elimu. "Tumepokea mradi wa kusambaza umeme kwa vijiji vilivyo pembezoni mwa miji, mradi huu unakwenda kutekelezwa vijiji tisa na vitongoji 34 kukamilisha umeme katika maeneo yote yaliyokuwa yanaonekana kuwa yametengwa," alisema.

Muragili aliipongeza REA kwa utaratibu mpya iliyojiwekea wa kuwaweka wazi wananchi miradi inayotekelezwa na kuwataka wananchi kutumia fursa hiyo ili kuepusha gharama za kuunganishiwa umeme majumbani.

# Majaliwa ataka mabalozi kuanzisha majukwaa ya kibiashara ughaibuni

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameagiza viongozi na watumishi katika balozi waendelee kufanya tathmini ya fursa za kiuchumi ambazo Tanzania inaweza kupata kutokana na ushirikiano wa kidiplomasia kwenye nchi walizoko.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa ubalozi wa Tanzania ulioko jijini Pretoria, Afrika Kusini.

Alisema ni vyema balozi hizo zikaanzisha majukwaa ya kiuchumi yatakayowakutanisha wafanyabiashara na wawekezaji wa nchi hizo katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo ardhi, madini, utalii, mawasiliano na biashara.

"Muwasihi wafanyabiashara na wawekezaji waje kuwekeza Tanzania na washirikiane na Watanzania kufungua makampuni, hii itatusaidia Watanzania kubadilishana uzoefu wa namna bora ya kuendesha biashara," alisema.

Waziri Mkuu alisema watumishi wa balozi za Tanzania hawana budi kuandaa makubaliano baina ya Tanzania na nchi walizoko ambayo yataonesha nini kinatakiwa nchini humo na ambacho kinapatikana kwa wingi nyumbani Tanzania.

"Hapa kwenu, ubalozi unapaswa kutengeneza makubaliano maalum ya kibiashara baina ya nchi hizi mbili na kubainisha aina ya bidhaa ambazo zinapatikana Tanzania kwa wingi na zinahitajika Afrika Kusini," alisisitiza.

Aidha, Waziri Mkuu alisema ni vyema pia ubalozi huo ukaendelea kuhamasisha watalii kutoka nchini humo kwa kubainisha vivutio vya utalii vilivyoko Tanzania ambavyo nchi hiyo haina huku akitolea mfano Mlima Kilimanjaro.

Awali, akitoa taarifa ya kiutendaji ya ubalozi huo, Kaimu Balozi Peter Shija alisema Tanzania inaweza kunufaika zaidi na fursa za biashara zilizopo nchini humo kwa kuuza mazao kama, mchele, maharage, korosho na mazao ya matunda.



Askofu Mkuu wa Kanisa la Elim Pentekoste Tanzania (KEPT), Peter Konki, wa kwanza(kulia) akipokea cheti cha ushindi wa uaskofu kutoka kwa aliyekuwa mwenyekiti wa uchaguzi Mwalimu James Masaay jana. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Mwandaaji vipindi wa East Africa Radio apata tuzo

**Na Mwandishi Wetu**

MWANDAAJI wa kipindi cha MamaMia kinachorushwa kila Jumatatu hadi Ijumaa saa 4:00 asubuhi hadi saa 6:00 adhuhuri na kituo cha redio cha East Africa, Anna Sombida, ameshinda tuzo ya Mwandaaji Bora wa Redio (Best Radio Producer).

Sombida alishinda tuzo hiyo juzi wakati wa utoaji wa Tuzo za Uandishi wa Habari za Watoto zilizotolewa na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF) Tanzania.

Akizungumza wakati wa utoaji wa tuzo hizo, Katibu wa TEF, Neville Meena alisema, moja ya sababu zilizofanya Sombida kupata tuzo hiyo ni kipindi chake kuwalenga zaidi wanawake.

Pia alisema, Sombida amekuwa akifanya na habari za watoto kwa kutoa elimu kwa jamii juu ya masuala mbalimbali yanayohusiana na watoto.

Kwa upande wake, Sombida alisema tuzo hiyo imempa nguvu na motisha ya kufanya kazi kwa bidii zaidi.

Alisema, kitendo cha kupata tuzo hiyo kimemwonyesha kuwa kazi anayoifanya inaonekana na ina nguvu kubwa, huku akiwashukuru TEF na UNICEF Tanzania kwa kutambua mchango wa waandishi wa habari katika jamii.

Pia alisema East Africa Radio ina mchango mkubwa katika kumkuza na kumfikisha hapo alipo kwa kuwa amekuwa akipewa nafasi ya kujifunza vitu vingi na kuongozwa vizuri kitu kilichosababisha kukomaa zaidi katika nafasi yake hiyo ya uandaaji wa vipindi.

Kutokana na tuzo hiyo, Sombida aliwataka waandishi wengine wa habari kutokata tamaa na kuchangamkia fursa pale zinapotokea, na ikitokea hawajafanikiwa wasikate tamaa kwa kuwa hata yeye hii si mara ya kwanza kushiriki katika tuzo hizo. Alisema mwaka jana alishiriki lakini hakufanikiwa kupata, hivyo amekuja kupata mwaka huu kwa sababu hakukata tamaa.

Kipindi cha Mama Mia kimekuwa kikiendesha kampeni mbalimbali zinazogusa jamii ikiwamo kampeni ya Mama Lishe ambayo kwa mwaka huu imewaongezea thamani mama lishe 25 katika wilaya tano za mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwapatia viwanja, majiko, friji na bidhaa zingine.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kanuni zitumike kusimamia maslahi ya wachezaji nchini

**WAKATI** dirisha dogo la usajili wa wachezaji wanaoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, First League na Ligi ya Wanawake Nchini likiwa wazi, kumeibuka sintofahamu kuhusiana na mkataba wa kiungo wa Yanga, Feisal Salum maarufu kwa jina la Fei Toto.

Kiungo huyo aliyezaliwa mwaka 1998 huko Unguja, Zanzibar alijiunga na Yanga akitokea Singida United (ingawa hakucheza mechi hata moja), ametangaza kuvunja mkataba wake na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Fei Toto ametangaza kuvunja na kuiaga klabu yake hiyo aliyoitumikia kwa mafanikio makubwa baada ya kuweka kiasi cha Sh. milioni 112 kwenye akaunti ya timu hiyo yenye maskani yake Mitaa ya Twiga na Jangwani kama matakwa ya kikatiba yanavyomtaka kufanya hivyo pale mchezaji atakapohitaji kuvunja mkataba.

Kati ya fedha hizo, Sh. milioni 100 ni ada ya usajili na kiasi kingine kilichobakia ni mishahara ya miezi mitatu (sawa na Sh. milioni nne kwa mwezi, mshahara ambao nyota huyo wa zamani wa JKU FC ya Zanzibar alikuwa akilipwa).

Huku kukiwa hakuna klabu yoyote au Fei Toto mwenyewe kuweka wazi wapi anataka kuelekea ama kwa kuhitaji kupata changamoto mpya au amevutiwa na maslahi bora aliyoahidiwa, Yanga imetangaza kurudisha kiasi chote cha fedha ambacho kiungo huyo alikiweka na kumtaka arejee kambini kujiandaa na michezo iliyoko mbele yao.

Unaweza kusema kama ni hadhithi au filamu inaandaliwa, lakini ukweli unabaki pale pale kila mchezaji au mfanyakazi yeyote anapenda kulipwa ujira ulio bora kulingana na kazi anayoifanya au majukumu aliyokabidhiwa na timu, taasisi au kampuni husika.

Inaweza kuonekana pia kama ni utovu wa nidhamu kwa mchezaji au mfanyakazi kuilipa ofisi iliyokuwa inamtumikisha, lakini katika dunia ya sasa mambo yamebadilika na kila upande unataka kuona haki inatendeka.

Fei Toto ni kama wachezaji wengine wa hapa ndani na nje ya Tanzania ambao wamewahi kujitokeza hadharani kudai maslahi bora au kuboreshewa mikataba yao na kuonekana wanakosea, lakini hili ni fundisho kwa viongozi wa klabu ambao wanafanya kazi kizamani.

Ni jambo lisilopingika wakati Fei Toto anasajiliwa Yanga haikufahamika kama atakuja kuwa mchezaji muhimu na tegemeo kwa timu, lakini ndani ya muda mfupi alionyesha uwezo na kipaji chake, hivyo viongozi wa Yanga walipaswa kukutana na kujadili kuhusu maslahi bora kama ambavyo imedaiwa nyota huyo alikuwa akiwaomba mabosi wake.

Tunashuhudia klabu mbalimbali za Ulaya zikiwaongezea wachezaji wake mishahara huku ikiwaongezea mikataba mirefu nyota wake, ni kwa sababu wamebaini kile ambacho walikuwa wakiwalipa wachezaji hao hakifanani na uhalisia wa huduma anayowapa lakini pia ikifanya mazungumzo ya kuwapunguzia mishahara au kuivunja kwa wengine waliobainika ni 'mizigo'.

Huku Yanga ikiamini jeuri iliyowekwa na mchezaji huyo aliyekuwa analilia kupewa mkataba mpya amepata wapi fedha za kuvunja mkataba uliokuwepo, klabu nyingine zisibweteke na zinatakiwa kujifunza kupitia makosa ambayo vinara hao wa Ligi Kuu wamekutana nayo.


Licha ya Yanga kutumia wadau wake mbalimbali kumbembeleza Fei Toto arejee kambini, lakini kiungo huyo ameendelea kushikilia msimamo wake wa kuondoka klabuni hapo na juzi wakati kikosi cha Nesreddine Nabi, kikielekea Morogoro kuwafuata Mtibwa Sugar, nyota huyo alionekana kwenye mazoezi ya timu ya JKU FC kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

Tunaamini hakuna jambo lisilokuwa na mwisho, huu ni wakati mwingine muhimu wa viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kulimaliza sakata hilo kwa kusimamia kanuni na taratibu zilizowekwa.

TFF inatakiwa kusimama kwenye weledi na kwa kufanya hivyo itawarudisha darasani viongozi wanaofanya kazi kwa mazoea lakini pia itawaamsha wachezaji kwa kuamini hakuna kinachoshindikana pale ukweli unaposimama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Suala la Fei Toto itumike sheria, busara na si nguvu

**SAKATA** la mchezaji, Feisal Salum na klabu yake ya Yanga ndilo linaloonekana kuzungumziwa zaidi kwenye masuala ya michezo kwa sasa na inaonekana ndilo linalofunga mwaka kwa kuongelewa kwenye sekta hiyo, kuanzia katika mitandao ya kijamii na hata vijiweni.

Feisal, maarufu kama Fei Toto kwa sasa yupo Zanzibar akiwa ameigomea klabu yake akidai maboresho ya maslahi zaidi.

Amekuwa akihusishwa na Azam FC, ikidaiwa klabu hiyo ipo nyuma ya pazia, lakini kwa kupitia Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Abdulkarim Amin 'Popat' amekanusha na kusema hata wao wanalisikia na kulisoma kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kama wengine.

Mengi yamezungumzwa na kujiri kwenye sakata hilo kama vile kuingizwa kwa fedha kwenye akaunti ya Yanga na wao wakairudisha katika akaunti ya mchezaji huyo.

Akaandika na barua ya kuaga klabu yake, lakini ikasema afuate taratibu zinazotakiwa na si ujanja ujanja.

Baada ya kuona hivyo, viongozi wa Yanga nao wakaandika barua kwenda Azam, ikiwa ni kama njia ya kujibu mapigo kuwataka wachezaji, Kipre Junior ambaye ni raia wa Ivory Coast na Mghana, James Akaminko.

Nadhani, kwenye mioyo ya viongozi wa Yanga wanajua kabisa Azam itakuwa nyuma ya mchezo huu.

Tamthilia iliendelea kwa Fei Toto kuonekana Zanzibar akiichezea timu yake ya zamani, JKU mechi moja ya kirafiki na kufunga bao.

Mpaka sasa hakuna chochote kinachoonekana kuendelea baina ya Yanga na mchezaji huyo. Mambo bado yako vilevile. Hii inaonyesha kila mmoja anajaribu kumtunishia msuli mwenzake na kila upande unajiona uko sahihi.

Kwangu binafsi naliona kama suala hili kwa nje linaonekana kama linakwenda vizuri na watu wanalizungumza kisiasa zaidi, lakini kwa ndani ni kinyume chake.

Pamoja na baadhi ya viongozi wa Yanga wanasema, Fei Toto ni kijana wao na watakaa ili waboreshe maslahi yake, lakini nadhani kuna tatizo.

Sidhani kama Fei Toto anaweza kukataa iwapo atapewa maslahi anayoyahitaji kwa sababu ndicho anachokitaka.

Pamoja na kudaiwa hakutumia njia inayokubalika kuwasilisha kilio chake, lakini klabu ingeweza kukaa naye na kumpoza.

Inawezekana klabu ilitumia nguvu za ushawishi iliyonayo kumlazimisha abaki badala ya mazungumzo ndiyo maana na yeye akaamua kufanya alichofanya.

Inawezekana Fei Toto anataka kurejea tena Yanga, lakini kile kitendo cha mashabiki kupiga kelele na kuimba hawamtaki kwenye mechi dhidi ya Azam kimemtisha na kuona kama akirejea anaweza asiwe tena kipenzi cha wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

Kwa uzoefu tu wa soka la Tanzania, viongozi wa klabu zenye mashabiki wengi hushindwa kabisa kuwadhibiti mashabiki wao wanapoamua kufanya jambo lao.

Inawezekana kabisa viongozi wa Yanga wakaendelea kumuona Fei Toto kama mkombozi na wanaweza kukaa naye na kumaliza tatizo, lakini kwa mashabiki wao wana lao moyoni na wanamwona kama msaliti, hivyo kujiweka kwenye wakati mgumu kama akirejea.

Miaka ya karibuni tu mchezaji, Metacha Mnata, alikumbana na kadhia hiyo, hivyo Fei Toto kwa sasa huenda anaona itamgeuka yeye.

Najua Yanga ni klabu kubwa na inatumia ushawishi wake ili kumbakisha kwa ajili ya kulinda heshima yake, lakini je ikifanya hivyo ustawi wa mchezaji utakuwaje kwa mashabiki na wachezaji wenzake?

Kwa maana hiyo, viongozi wa Yanga jambo ambalo wanatakiwa wafanye ni kuwapoza mashabiki wao ili kwanza wamuone Fei Toto si mkosaji na msaliti, bali alikuwa anatetea maslahi yake.

Hiyo itamfanya mchezaji huyo kutohofia kurejea, wakati huo ikitengeneza maboresho ya maslahi ya mchezaji mwenyewe anayoyahitaji.

Hapo itakuwa imefanikiwa badala ya kutumia nguvu ya ushawishi wa klabu kubwa. Kama mchezaji akigoma kabisa, basi viongozi ama watumie sheria ili klabu kupata haki yake na si vitisho, lakini pia busara inatakiwa. Wakiona kama wanaweza kumwacha aende basi wafanye hivyo ili akili yao ijielekeze kwenye mambo mengine ya maendeleo ya klabu badala ya sakata la Fei Toto kila kukicha kama tamthilia.

# Askofu asisitiza malezi ya upendo

**Na Elizabeth Zaya**

ASKOFU wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga, Mhashamu Liberatus Sangu, amewataka wazazi, walezi na jamii kuwalea watoto katika misingi ya utu, upendo na maadili mema, ili yasaidie kupunguza vitendo vya ukatili vinavyofanyika sasa.

Askofu Sangu alitoa kauli hiyo wakati wa mahubiri yake, katika Misa ya kumbukumbu ya watoto Watakatifu Wafia Dini, ambayo imefanyika kijimbo katika Kanisa kuu la Mama Mwenye Huruma, Ngokolo mjini Shinyanga.

Kiongozi huyo wa kiroho aliwataka Watanzania kuungana kukabiliana na vitendo vyote vya ukatili kwa watoto kutokana na madhara yake kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Alisema watoto wanaolelewa katika mazingira ya ukatili huendeleza vitendo hivyo pale wanapokuwa watu wazima, kwa sababu mbegu ya ukatili hupandikizwa na kukua ndani mwao tangu ututoni.

Pia aliwataka watoto kuwaheshimu wazazi kama njia ya kumtangaza Kristo, ambaye ni upendo, kuwapenda na kuwatendea mema watu wengine.

Alisema Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga limeamua kufanya maadhimisho hayo ambayo huadhimishwa kila mwaka mwezi huu yakiwa na ujumbe maalum wa kupinga ukatili kwa watoto, ikiwa ni hatua ya kuunga mkono juhudi za serikali pamoja na wadau wengine.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alisema ni vyema wazazi, walezi na jamii nzima kuhakikisha watoto wanalindwa dhidi ya maovu wanayofanyiwa, pamoja na kuwapa haki sawa bila kuwabagua kwa misingi ya kijinsia.



Kundi la wakazi wa mjini wa Muheza mkoani Tanga wakipigana vikumbo na kutishiana kupigana ngumi jana asubuhi wakati wakigombea maziwa ya msaada ambayo yalikuwa yanatolewa bure katika kituo cha kukusanyia maziwa kwa wafugaji kilichopo eneo la Tanesco barabara kuu ya Muheza-Pangani. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waziri apiga marufuku shughuli katika maeneo hifadhi za misitu

**Na Munir Shemweta,** LINDI

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amepiga marufuku shughuli za kibinadamu katika maeneo ya hifadhi ya msitu wa Nyengedi na Pori la Akiba la Selous mkoani Lindi.

Mabula alipiga marufuku hiyo juzi wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mtepera wilaya ya Kilwa mkoa wa Lindi wakati wa ziara ya kamati ya mawaziri wanane wa wizara za kisekta mkoni hapa ikiwa ni utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.

Uamuzi huo wa Dk. Mabula anayeongoza timu ya mawaziri wa wizara za kisekta, unatokana na maelekezo ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack, baadhi ya wananchi wamekuwa na tabia ya kufanya shughuli za kibidamu kwenye maeneo ya hifadhi ya msitu wa Nyengedi na Pori la Akiba la Selous wakati wana maeneo ya kutosha kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

Dk. Mabula alivitaja vijiji ambavyo wananchi wake wamekuwa na tabia ya kutoka maeneo yao na kwenda kufanya shughuli za kibinadamu katika eneo la hifadhi kuwa ni Chiodya B, Chiodya A, Mihango, Ntauna, Mnara, Mtakuja, Chikombe na Mkanga vilivyoko hifadhi ya msitu wa Nyengedi.

Vijiji vingine ni Mtepera, Zinga Kibaoni na Kikulyungu vilivyopo Hifadhi ya Pori la Akiba Selous. "Kijiji hiki cha Mtepera kina eneo kubwa ambalo halijatumika vizuri. Mto Matandu ni chanzo cha maji na unaanza kupoteza sifa kwa sababu tu ya shughuli za kibinadamu ziko karibu. Wananchi wa eneo hilo hawastahili kabisa kuwa karibu na vyanzo vya maji," alisema.

Mapema, wakati Kamati ya Mawaziri Nane wa Wizara za Kisekta walipokutana na uongozi wa mkoa wa Lindi, Telack alisema katika kushughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi, mkoa wake umebaini baadhi ya wananchi kuingia maeneo ya hifadhi na kufanya shughuli za kibinadamu, hivyo kuathiri ikolojia ya eneo la Mto Matandu.

Alisema mto huo ni muhimu na wenye faida kubwa kutokana na kuwa sehemu ya mito inayopeleka maji kwenye mradi mkubwa wa bwawa la Mwalimu Nyerere, Rufiji.

Kwa mujibu wa Telack, mkoa wa Lindi umetenga maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwamo ufugaji, hivyo akawataka wananchi wa maeneo hayo kuanza kuchimba malambo na kubaki katika maeneo yaliyotengwa.

Mawaziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Khamis Hamza Chilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, walisisitiza umuhimu wa wananchi wanaoishi karibu na hifadhi kuacha kuvamia na kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya hifadhi kwa kuwa shughuli hizo zinaleta athari za kimazingira ikiwemo kuharibu vyanzo vya maji.

Timu ya Mawaziri nane wa Wizara za kisekta inaendelea na ziara katika mikoa mbalimbali nchini kwa lengo la kupeleka mrejesho wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.

# Mambo yaanza kuiva mwendokasi Mbagala

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amefungua barabara ya juu ya Kilwa katika mradi wa mabasi yaendayo haraka kutoka Stesheni/Gerezani hadi Mbagala yenye urefu wa kilomita 20.3.

Akizungumza baada ya ufunguzi jana, Dar es Salaam, Prof. Mbarawa alisema awamu itakayofuata sasa ni kufungua barabara kama hiyo eneo la Bandari na Chang'ombe, ikiwa ni mwendelezo wa kupunguza msongamano mkoani Dar es Salaam.

Prof. Mbarawa alisema kwamba baada ya ujenzi wa barabara hiyo kukamilika itafuata awamu ya kilomita 17 kutoka Mbagala Mwisho hadi Vikindu, kuanzia mwaka 2023/24 kutokana na kubaini kwamba eneo hilo lina foleni kubwa.

"Lengo letu ni kupunguza foleni kwa watumiaji wa barabara kutoka mjini hadi Mbagala, tunafahamu wakazi wa Temeke, Mbagala walikabiliwa na changamoto hii kwa muda mrefu. Leo (jana) magari kuanza kupita barabara ya juu ni hatua kubwa," alisema Prof. Mbarawa.

Awali, Meneja Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili, Mkoa wa Dar es Salaam, Mhandisi Barakael Mmari, alisema barabara hiyo imekamilika kwa asilimia 82 na kwamba ikikamilika itakuwa na vituo 27.


Mmari alisema mradi huo wa Dar es Salaam, unahusisha madaraja ya juu manne ambayo ni Bandari, Kilwa, Chang'ombe na Kawawa na kwamba ufunguzi wa barabara hiyo jana, utaruhusu mkandarasi kuendelea na ujenzi barabara ya chini kwa kuweka zege.

"Ufunguzi wa barabara ya juu hii leo (jana) ni mwendelezo wa barabara ya chini kwa zege ambayo itakauka kwa siku 28, kisha kuruhusu magari kupita tena chini," alisema.

Mbunge wa Mbagala, Abdallah Chaurembo alisema wakazi wa Temeke na Mbagala, wanamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa fedha kuruhusu miradi ya maendeleo ikiwamo wa Mabasi Yaendayo Haraka.

Alisema wakazi wa eneo hilo walipata changamoto ya foleni kwenye eneo hilo takribani miaka 15, akisema sasa shughuli za kiuchumi zitafunguka kwa kuwa usafiri utakuwa wa haraka.

RIPOTI MAALUM




# Mbwa mwitu; bidhaa ipatikanayo Afrika pekee, hatarini kutoweka

INATOKA Uk. 4

"Wana masikio makubwa, pua ndefu, miguu mirefu na vidole vinne kwenye kila mguu. Kundi la mbwa mwitu linaweza kuwa na idadi ya wanyama 10 hadi 30, huwasiliana baina yao kwa njia kugusana, sauti na mijongeo.

"Endapo mmoja atatoweka kwenye kundi na kurudi baadaye, wenzake humuua kwani huja na harufu nyingine, hivyo hana budi kukimbia na kwenda kuanza maisha mapya kwingineko.

"Mbwa mwitu ni miongoni mwa wanyama ambao humla mnyama waliyemwinda akiwa bado anapumua. Kimo cha mbwa mwitu hufikia hadi inchi 30 (futi tatu), urefu wake hufikia inchi 30 hadi 56 (futi 3-5) na uzito hufikia Kg 18 hadi 25.

"Hawa ni miongoni mwa jamii ya wanyama walao nyama na hupendelea sana kuwinda wanyama wa maumbo ya kati kama swala pala, pongo, swala tomi na ngiri.

"Mara tu baada ya kupandana, mbwa mwitu jike hukaa na mimba kwa takribani siku 70 (miezi miwili na siku 10) kisha huzaa kuanzia watoto wawili hadi 20 na kubaki anawachunga ndani ya wiki chache mpaka watakapoweza kujitegemea. Huwategemea wenzake ndani ya kundi kwa ajili ya chakula. Maisha ya mbwa mwitu katika maeneo yake ya asili hufikia miaka 10 hadi 12.

"Wanyama hawa hawapatikani sehemu nyingine yoyote duniani zaidi ya Bara la Afrika na ni nchi chache tu za Afrika utaweza kuwaona. Kwa mujibu Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na uhifadhi wa maumbile asili (IUCN), mbwa mwitu ni wanyama waliyo hatarini kutoweka duniani," anafafanua.

Mtaalamu huyo anashauri kulindwa maeneo ya mapito ya wanyamapori (shoroba) ili kuongeza uwezekano wa mbwa mwitu kuzaliana, pia jamii ipewe elimu kuepuka mauaji ya wanyamapori hao kutokana na migogoro inayoendelea baina ya wanyamapori na binadamu.

"Kuanzishwe mbinu mbalimbali ambazo zitasaidia kulinda makundi madogo ya mbwa mwitu hasa kutokana na magonjwa ambayo yanaonekana kuwa tishio kwa wanyamapori hawa.

"Pia ufanyike utafiti mara kwa mara ili kugundua maeneo yanayoathirika zaidi na uharibifu wa mazingira na kuathiri ongezeko la wanyamapori hawa ili kutanua uga kwa ajili ya mtawanyiko na kuzaliana kwa mbwa mwitu.

"Vilevile, kuwe na ufuatiliaji wa mara kwa mara wa uelekeo wa wanyamapori hawa na kujua baadhi ya magonjwa mengine yanayozuka ili kuyadhibiti kabla hayajaleta madhara kwao na kupunguza kasi ya kuongezeka kwao.

"Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na mamlaka za uhifadhi wanyamapori, kwa pamoja wasaidiane kuanzisha maeneo maalumu kwa ajili ya kuwafuga wanyama hawa ili wazaliane na kuongeza idadi yao na kisha kuwapeleka kwenye hifadhi," Omary anashauri.

**MTAFITI WANYAMAPORI**

Mtafiti wa Wanyamapori, Emanuel Sisya anaunga mkono mapendekezo ya mtaalamu Omary, akiwa na angalizo kwamba wanyama hao kwa sasa wamebaki takriban 6,600 (wakubwa wasiozidi 1,400), wakiwa kwenye maeneo machache yaliyohifadhiwa Afrika Kusini na kusini mwa Afrika Mashariki, hasa Tanzania na Kenya (Mbuga ya Savo) pamoja na kaskazini mwa Msumbiji.

"Kwanini tuwahifadhi mbwa mwitu? Ni wanyama ambao wapo hatarini kupotea na wana uwezo wa kuwinda wanyama mbalimbali na kufanikiwa kwa zaidi ya asilimia 75 kupata kitoweo.

"Katika uwindaji huu tunasema wanaondoa wanyama dhaifu na wagonjwa katika mfumo wa ikolojia, wanyama hawa huondoa uchafu na kula mizoga. Kwa ujumla, husaidia kuuweka sawa mfumo wa chakula na hivyo kuhuisha mfumo wa asili wa kiikolojia.

"Wanyama hawa wanatembea umbali mrefu kwa kasi ambayo ni takribani maili 35 kwa saa moja na wanaishi kwa makundi, hivyo kuwawezesha kujitafutia chakula kwa urahisi na kuendeleza maisha yao. Ni wanyama ambao wanavutia sana kwa shughuli za utalii," Mtafiti Sisya anabainisha.

Kama ilivyo kwa watangulizi wake, Mtafiti Sisya anashauri elimu itolewe kwa wananchi kulinda wanyamapori na mapito ya wanyama hao katika kufanikisha uendelevu wa mfumo wa kiikolojia.

"Serikali iendelee kushirikiana na mashirika ya uhifadhi na wadau mbalimbali wa uhifadhi ili kuleta miradi inayolenga kuinua maisha ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa maeneo yaliyohifadhiwa au mapito ya wanyama kwa lengo la kutengeneza dhana ya ushirikishwaji katika uhifadhi wa mbwa mwitu ili waendelee kuwapo na kuitajirisha nchi yetu kwa kuiingizia kipato na kuonwa na vizazi vijavyo," Mtafiti Sisya anashauri.

Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia hotuba yake ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka huu wa fedha (2022/23) inabainisha mikakati yake katika kukabiliana tishio la kutoweka kwa mbwa mwitu, ikieleza kuwa kupitia TAWIRI inawafunga mikanda ya mawasiliano baadhi ya wanyamapori, wakiwamo mbwa mwitu wa Mfumo wa Ikolojia ya Serengeti ili kuainisha mienendo yao katika vipindi mbalimbali na maeneo yenye migogoro (conflict hotspots) pamoja na kupendekeza njia sahihi za kutatua migogoro hiyo.



Baadhi ya mbwa mwitu wakiwa ndani ya boma kwenye eneo la Mradi wa Uzalishaji wa Mbwa Mwitu katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi.

# Wafanyabiashara Samunge wapata matumaini

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

BALOZI wa Amani Afrika, Dk. Geordavie Kasambale, ameahidi kuwashika mkono wafanyabiashara wadogo wa Soko la Samunge (NMC) lililoko jijini Arusha, ambalo liliteketea kwa moto na kusababisha hasara ya mali na bidhaa mbalimbali.

Ameahidi kuwapatia fedha za mitaji na kuwatengenezea miundombinu mipya ndani ya soko hilo lililoungua moto mwaka 2020.

Dk. Kasambale ambaye pia ni Nabii Mkuu wa Kanisa la Ngurumo ya Upako, aliahidi kutekelezwa agizo hilo jana.

"Nilipokea barua kutoka Kwa wafanyabiashara wadogo (machinga) wa Soko la Samunge, wakiwa wanataka msaada wa vitu mbalimbali ikiwemo mitaji na kujengewa miundombinu ya soko hilo.

"Napenda niwaambie sitawaacha hivi hivi, nimekubali na nitaenda sokoni hapo kwa ajili ya kuwasaidia."alisema Nabii Mkuu, Dk. Kasambale.

Baada ya ahadi hiyo, Mwenyekiti wa Soko la Samunge, Mraji Njola, alisema wao kama wafanyabiashara wadogo walikaa chini na kuamua kumuandikia barua, Dk. Kasambale kumwomba msaada wa miundombinu ya soko ikiwemo milango ya bati na chuma,mitaro pamoja na mitaji.

"Mwaka 2020 tuliunguliwa na soko hili na wafanyabiashara wengi walipoteza mitaji yao. Sisi unavyotuona tumeanza upya na hatuna mitaji. Soko letu halina miundombinu kama mageti, ambayo kama yatawekwa yatasaidia kupunguza wizi unaotokea mara kwa mara.

"Katika soko hili kuna wanawake wengi ambao ni wajane wanaotegemea kufanya biashara ili waweze kulea familia zao. Wengi wao walipoteza mitaji kipindi kile ambacho soko liliungua," alisema.



Mkurugenzi Mkuu, Wakala wa Nishati Vijijini, (REA) Mhandisi Hassan Saidy wa kwanza kushoto akizungumzia namna miradi ya REA ilivyotekelezwa mara walipokutana na viongozi wengine katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga kupanga mpango wa makabidhiano ya mikataba jana, katikati ni Mkuu wa Wilaya ya Tanga Hashimu Mgandilwa akifuatiwa na Kaimu Meneja wa TANESCO Mkoa wa Tanga Mhandisi William Masome. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

# Wataka Samia kutenga siku kuhamasisha unywaji maziwa

**Na Hamida Kamchalla,**

TANGA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameombwa kutenga siku maalum kila mwaka katika kalenda yake ambayo itatumika kuhamasisha wananchi kuhusu unywaji wa maziwa.

Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Yussuf Hassan, alisema janak uwa ombi hilo linatokana na kiwango cha unywaji wa maziwa kuwa chini ya viwango vinavyoelekezwa kimataifa.

Kamati hiyo ilikuwa jijini Tanga kujifunza na kubadilishana uzoefu juu ya maendeleo ya ufugaji.

Aidha, Kamati hiyo ilianza kwa kuitembelea Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) na Kiwanda cha Kusindika Maziwa cha Tanga Fresh

"Niwaombe viongozi wangu wa kitaifa kwa pande zote mbili (Tanzania Bara na Zanzibar), kama itawapendeza kutenga siku moja tu ndani ya siku 365 ambayo itakuwa maalumu kuifanya iwe siku ya uhamasishaji wa unywaji wa maziwa kwa wananchi." alisema.

Mwenyekiti huyo aliwasisitiza wafugaji na wadau wanaofanya biashara ya maziwa na Kiwanda cha Tanga Fresh, wasikate tamaa ya kupeleka mazao yao ya Mifugo hasa maziwa, badala yake wafanye makubaliano na kupeleka kwa wingi ili uzalishaji uongezeke tofauti na ilivyo sasa.

"Tumeafikiana kwamba soko la maziwa lipo kubwa, hivyo wafuge kisasa zaidi ili waweze kupata maziwa mengi, na kiwanda hiki kinahitaji maziwa ya kutosha, tumeona kwasasa maziwa siyo mengi na ndiomaana uzalishaji siyo mkubwa" alisema.

Katika ziara hiyo ya mafunzo, Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo (SMZ), Shamata Shaame Khamis, alisema mbali na ziara hiyo kuwafunza mambo mengi, lakini pia wamefurahishwa na mapokezi waliyopata kutoka kwa viongozi wa Mkoa.

"Moja ya vitu tulivyojifunza katika ziara hii kwanza ni jinsi ya Taasisi za Utafiti zinavyofanya kazi zake katika kuongeza kiwango cha uzalishaji hii itamsaidia mkulima wa Tanzania kuweza kuzalisha kwa kiwango kikubwa cha ubora.

"Viongozi wetu wa serikali zote mbili wanakaa na kutuelekeza tufanye kazi kwa ushirikiano wa hali ya juu, na lengo ni kuona kuwa sekta tunazoziongoza zinaendelea kunufaisha wananchi katika kujiongezea kipato," alisema.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Hashimu Mgandilwa, alisisitiza ufugaji wa kisasa ili kuweza kuleta tija katika uzalishaji badala ya kufuga kimazoea huku uzalishaji ukiwa mdogo

# Vijana wapokea pikipiki, mashine kwa ujasiriamali

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Meru iliyoko mkoani Arusha, imekabidhi pikipiki 18 zenye thamani ya Sh. milioni 45 na mashine ya kutotolea vifaranga vya kuku yenye thamani ya Sh. milioni nane, kama njia mojawapo ya kuwainua kiuchumi vijana wa Meru.

walionufaika na uwezeshaji huo ni vikundi vitatu vya vijana, vilivyotimiza sifa za kukopeshwa kupitia fedha za makusanyo ya ndani.

Mbunge wa Arumeru Mashariki, Dk. John Palangyo, alisema mkopo huo wa vijana ni sehemu ya Sh.milioni 237 zilizotolewa na Halmashauri hiyo katika robo ya kwanza kwa mwaka huu wa fedha.

Akikabidhi pikipiki hizo jana, Dk. Pallangyo aliwaelekeza vijana hao kutumia vizuri vyombo hivyo na kuzitunza ili kujikwamua kiuchumi.

"Lakini halmashauri imenunua vyombo hivi kwa mapato yake ya ndani, hivyo lazima mkavitunze na kuzingatia sheria za usalama barabarani, ili kuwa na afya njema kwa kuepuka ajali zitokanazo na uzembe,"alisema.

Alisema anaamini wakivitunza vyombo hivyo watajiinua kiuchumi na kuinua uchumi wa familia na taifa.

Pia Dk. Pallangyo, alikabidhi vyereani vitatu kwa kikundi cha vijana 'Old is Gold Youth Group kutoka toka Usa River. Vyerehani hivyo ni ufadhili kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu.


Kabla ya makabudhiano hayo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Meru, Jeremia Kishili, alisema halmashauri hiyo itaendelea kukusanya mapato na kuwaletea wananchi maendeleo ili kila mmoja anufaike nayo.

"Lakini natoa wito kwa waendesha pikipiki kuwa waadilifu na kutumia vyombo hivi kujiletea maendeleo na siyo kuvitumia vibaya na kusababisha ajali zitakazopoteza uhai wenu na wengine au kusababisha ulemavu wa maisha," alisema.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Zainabu Makwinya, alisema ushirikiano kati ya waheshimiwa madiwani na wataalam umesaidia kuhakikisha mapato yanakusanywa na kuwaletea wananchi maendeleo, kupitia utoaji wa mikopo isiyo na riba, utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Makwinya pia alisema licha ya halmashauri kutoa mkopo wa pikipiki kwa vijiana na mashine ya kutotolea vifaranga, lakini pia aliomba Ofisi ya Waziri Mkuu kutoa vifaa kama cherehani kwa vijana, ili wajiajiri na kujikwamua kiuchumi.

Akisoma taarifa kuhusu vifaa hivyo, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Meru, Flora Msilu, alisema vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh.milioni 53 ( pikipiki 18 na mashine ya kutotolesha vifaranga), vimenunuliwa kupitia mapato ya ndani.





# Hekta 23 TPC zateketea kwa moto

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TAKRIBAN hekta 23 za ardhi zilizoko ndani ya Ranchi ya Wanyamapori ya TPC, Moshi mkoani Kilimanjaro, zimeteketezwa kwa moto na watu wasiojulikana, baada ya kuichoma ranchi hiyo kwa makusudi ya kuharibu ikolojia na kudhuru wanyamapori.

Hadi sasa haijajulikana ni wanyamapori wangapi walioko katika ranchi hiyo wameathiriwa na moto huo, ingawa menejimenti ya Kampuni ya Sukari ya TPC, imethibitisha kuwa hilo ni tukio la pili kwa mwaka huu.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Simon Maigwa, tukio hilo la kuteketeza moto ranchi hiyo lilifanyika juzi majira ya usiku.

Akiwasilisha taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kuhusu hujuma hiyo, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu na Utawala, Wakili David Shilatu, alisema mpaka sasa wahusika waliofanya hujuma hiyo hawajajulikana.

"Katika ranchi hii wako wanyamapori ambao ni nyara za serikali kwa ajili ya kuvutia watalii. Kilichofanyika hapa ni hujuma za waziwazi. Hatuna ubaya na mtu ila kama kuna wananchi, yapo mambo ambayo wanayaona hayaendi sawa, waje kwetu waonane na viongozi wa kiwanda ili kujadili mambo hayo na kupatiwa ufumbuzi.

"Hawa wananchi wanaotuzunguka tunawajali kwa mambo mengi, mfano Kata ya Arusha Chini, tumeongeza bajeti ya huduma ya jamii, ambapo tunatekeleza miradi mbalimbali ya afya, elimu na mingineyo. Lengo letu ni kuhakikisha wananchi wanaozunguka kiwanda wananufaika na kiwanda." alisema Shilatu.

Akizungumza baada ya kuzuru eneo hilo, Mkuu wa Mkoa huo, Nurdin Babu, alisema: "Nitumie nafasi hii kama serikali kuwaonya wale wote waliofanya vitendo hivi kuacha mara moja. Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinaendelea kuchunguza ili kuwabaini waliofanya matukio haya na kujua sababu ya kufanya matukio hayo pamoja na kuchukuliwa hatua kali za sheria."

Mkuu huyo wa mkoa alisema kiwanda hicho kimekuwa na ushirikiano mzuri na wananchi wanaozunguka kiwanda hicho kwa kusaidia miradi mbalimbali ya maendeleo, hivyo kukihujumu ni kinyume cha sheria.

"Nitakuja kufanya mkutano na wananchi mnaozunguka kiwanda hiki ili mnieleze kama mna mambo yenu ambayo kiwanda hakijawatimizia ili tuweze kukaa na viongozi wao na kujua nini shida hapa.

"Nataka tujenge mahusiano mazuri kumbukeni humu ndani kuna wanyama mbalimbali ambapo watalii wanafunga safari makwao kwa ajili ya wanyama hawa," alisema Babu.



Mkurugenzi wa Chuo cha Uuguzi cha Elljerry na kituo cha biashara cha Msekwa Park kilichopo barabara kuu ya Muheza - Amani wilayani Muheza mkoani Tanga Elizabert Chigua kushoto akitoa maelekezo wakati akishiriki na wananchi kupanda miche ya miti ya kutunza mazingira jana katika kituo hicho cha biashara cha Msekwa Park ambapo zaidi ya miti 100 itapandwa eneo hilo mwaka mpya 2023, Wapili kulia aliyesimama ameshika mti msimamizi wa shughuli hiyo Salimu Bendera. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wawekeana maazimio kumalizia mgogoro wa wakulima, wafugaji

**Na Anjela Mhando,** SIHA

AMRI ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ya kuitaka wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, kumaliza migogoro ya malisho ya mifugo kati ya wafugaji wa jamii ya Kimasai na wakulima, imetekelezwa kwa mafanikio makubwa baada ya kuwekeana maazimio.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Thomas Apson, alikutana jana na makundi ya wafugaji na kuweka masharti magumu ya namna ya kuepusha migogoro, ambayo huingiza pande hizo mbili katika vurugu na kutishia kutoweka kwa amani.

Akizungumza katika kikao hicho, Apson alisema katika masharti hayo mapya, amewaelekeza wafugaji kuboresha ufugaji wao na kufuga kisasa ili kumaliza migogoro ya aina hiyo inayotokea mara kwa mara.

"Masharti mengine ni pamoja na kufanyika sensa ya mifugo ili kubaini idadi ya wafugaji walioko Siha ni wangapi na mifugo ni mingapi. Idadi hiyo ya wafugaji itatusaidia kutengeneza mfumo ambao utasimamiwa na maofisa watendaji wa vijiji na wenyeviti wa vijiji na vitongoji."Kwamba kila mgeni akiingia mpya na mifugo yake, ni lazima aripoti kwenye serikali ya eneo husika ili ijue mifugo mingapi imeingia na imekuja kufanya nini na itakaa kwa muda gani."alisema.

Aidha, serikali imeongeza masharti mengine ambayo ni kuilazimisha Halmashauri ya Wilaya hiyo, kutenga maeneo ya malisho ya mifugo au kubainishwa maeneo maalumu kwa ajili ya wafugaji.

"Tunafanya hivyo, kwa maana ya kuzingatia ule mfumo wa serikali wa matumizi bora ya ardhi. Hapa maana yake ni kwamba Wilaya inakuwa na maeneo tengefu ya kilimo na ya wafugaji, lakini pia yajulikane maeneo ya makazi," alisisitiza.

Ofisa Kilimo na Uvuvi, Dk. Barnabas Mbwambo, akizungumza katika kikao hicho, alisema yako maelekezo mengine madogo hasa kwenye suala la udhibiti wa vyanzo vya maji ambalo linaenda sambamba na lile la kutenga maeneo ya malisho na tunaendelea vipi kuvitunza, lakini pia kuwepo na kamati ndogo ambayo itakuwa inafanya maridhiano kunapokuwa na migogoro hiyo.

Akitolea ufafanuzi suala la utambuzi wa mifugo, Mbwambo alisema hayo ni maelekezo ya serikali na kwamba kila Wilaya imeagizwa kutambua mifugo yake, idadi na wafugaji wenyewe.

Amri hiyo ya Waziri Mkuu Majaliwa, iko kwa mujibu wa Sheria ya Mifugo Namba 12 ya Mwaka 2010, ambayo pamoja na mambo mengine inazungumzia usajili ufumbuzi na ufuatiliaji wa mifugo.

Baada ya kutangazwa masharti hayo, baadhi ya wafugaji, Jeremia Laizer na Simel Kitasho, kwa nyakati tofauti walisema maelekezo ya serikali hayana namna ni lazima yafuatwe ili kuepuka mkono wa sheria.

Kitasho alisema yeye amepokea maelekezo hayo ya Waziri Mkuu na kwamba ana hakika hakuna mfugaji atakayekaidi amri hiyo zaidi ya kutoa ushirikiano kwa serikali na kuhakikisha mifugo yao inahesabiwa.

# Walimu waombwa kujiunga chama kutetea haki zao

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

KAIMU Katibu wa Chama cha Kulinda na Kutetea Haki za Walimu (CHAKUHAWATA) Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Constantine Tunch, amewasihi walimu kujiunga na chama hicho kwa kuwa kina manufaa kwao, ikiwamo kutetea haki na stahiki zao.

Alitoa rai hiyo jana, wakati akizungumza na wanahabari kuhusu mikakati mbalimbali ya kuimarisha chama hicho kuwatetea walimu katika eneo hilo.

Tunch alisema hadi sasa hivi chama hicho, wilayani humo kina wanachama 62 kutoka shule mbalimbali waliyojiunga kupitia matawi yao.

"CHAKUHAWATA kuna maslahi makubwa na mwanachama atakatwa Sh.5,000 pekee kwa mwezi tofauti na vyama vingine vinavyokata asilimia mbili ya mshahara kwa kila mwezi," alisema Tunch.

Hata hivyo, alisema wanachama wao ni walimu hivyo hawachagui mwalimu wa shule ya sekondari au msingi na wanamshukuru mwajiri wao kwa kuwapa nafasi walimu ya kujiunga na chama wanachokipenda.

"Katibu Mkuu wa CHAKUHAWATA, aliandika barua ya kutambulisha chama chetu, mkoani Manyara Aprili mosi mwaka huu wa 2022 hivyo walimu wasiwe na hofu ya kujiunga nasi," aliongeza Tunch.

Pia alisema chama hicho, kinatambuliwa kwa kuwa kimesajiliwa kwa mujibu wa sheria ya ajira na mahusiano kazini ya mwaka 2004 kifungu cha 48 na kifungu kidogo cha (5).

"Chama chetu kina kanuni, katiba na hati ya kusajiliwa hivyo walimu wajiunge kwa kuwa tunamuheshimisha kujiunga na chama anachokitaka kwa kuwa kina uwezo wa kusimamia na kutetea maslahi ya walimu," alisema.

Vilevile, alisema chama katika eneo hilo, Simanjiro kinakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwemo baadhi ya walimu kukosa ufahamu juu ya sheria ya ajira na mahusiano makazini.

"Kutofahamu sheria kumesababisha baadhi ya walimu kuwa na hofu na uoga hivyo kudhani kuwa wakijiunga na chama hiki watakuwa wamemkosea mwajiri wao kumbe sivyo,"alisema.

Alisema walimu hawafahamu mipaka au tofauti ya mwajiri na chama cha wafanyakazi, kwa kuwa mwajiri hawezi kuwachagulia kuwa wanachama wa chama cha kuwatetea zaidi ya wao wenyewe kuamua.

"Pia chama hakijaimarika kiuchumi kwa kuwa bado hatujatoa ajira kwa nafasi zinazotakiwa na hatujafika maeneo mengi ya Wilaya ya Simanjiro katika kuwafikia wanachama," aliongeza Kaimu Katibu huyo.





# RC awabana ma-DC na ma-DED upandaji miti

**Na Peter Mkwavila,**

DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule amewataka wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri zote mkoani hapa kutumia fursa ya kipindi hichi cha mvua kupanda miti kwenye maeneo yao ili kutunza mazingira na kuweka jiji katika hali ya usafi.

Rosemary alitoa maagizo hayo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti mkoani hapa inayotarajiwa kuanza kutekelezwa leo.

Alisema mkoa umejipanga kupanda miti katika kipindi hiki cha mvua, hivyo ni vyema wakazi wote wa mkoa kushiriki kupanda miti kwa wingi ili kwenda sambamba na nia Rais Samia Suluhu Hassan ya 'kuikijanisha' Dodoma.

Mkuu wa Mkoa alitoa wito kwa wananchi kuhakikisha wanapanda miti isiyopungua mitano kwenye maeneo ya makazi yao ikiwamo ya matunda na kivuli.

"Tumedhamiria kuwa na kampeni ya upanadaji miti jijini Dodoma ili kutimiza lengo la kamapeni ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani, hivyo serikali kupitia wadau na taasisi mbalimbali, imeona ni vyema kuendelea juhudi za kuufanya Mkoa wa Dodoma kuwa na miti ya kutosha," alisema.

Mkuu wa Mkoa alisema kutokana na kuanza kwa msimu wa mvua, ni wakati sahihi kwa wanachi wote kuanza kutekeleza kampeni hiyo ya kupanda miti katika maeneo yao kuanzia ngazi ya kaya, kata hadi wilaya.

"Kwa msisitizo mwaka huu wananchi wahakikishe kuwa miti yote ambayo itapandwa inastawi na kukua vizuri, ni dhahiri kuwa miti ina mchango mkubwa katika maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla kwani misitu inatoa asilimia 45 ya malighafi za ujenzi.

"Misitu pia hutumika kunyonya hewa ukaa, kutupatia hewa safi, kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji, pia hutupatia Pato la Taifa na mtu mmoja mmoja na maisha ya mwanadamu hutegemea misitu tangu kuzaliwa hadi ukomo wa maisha yake," ali-

# Bilioni 580/- zatumika kusaidia walengwa TASAF

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

ZAIDI ya Sh. bilioni 580 kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) zimetumika kulipa walengwa wa kaya maskini tangu kuanza kwa kipindi cha pili cha mpango wa kunusuru kaya hizo mwaka 2020.

Kaya mpya zaidi ya 200,000 zinatarajiwa kuingia kwenye mpango huo baada ya kukamilika taratibu za kuzipata.

Mkurugenzi Mkuu wa TASAF, Ladislaus Mwamanga alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema Sh. bilioni 580.297 zimetumika katika miaka miwili na nusu ya utekelezaji wa kipindi cha pili cha mpango huo.

Alisema kuwa katika mpango wa kwanza wa kunusuru kaya maskini ulioanza mwaka 2012, hadi kufika mwaka 2019 ulikuwa na kaya za walengwa 1,118,752 ambazo zilitambuliwa kutoka asilimia 70 ya vijiji, mitaa na shehia zote nchini.

Pia alisema kipindi cha pili cha awamu ya tatu kilichoanza Februari 2022 umeongeza kaya lengwa hadi kufikia 1,371,038 zenye watu zaidi ya milioni tano ambao ni asilimia 55 ya kaya zinazoishi kwenye mazingira magumu nchini.

Mwamanga alisema kuwa baada ya kukamilika kwa mchakato wa kuzitambua kaya maskini, zaidi ya kaya 200,000 zinatarajiwa kuingizwa kwenye mpango huo.

Alisema hatua hiyo inafuatiwa na kazi ya kuondoa kwenye mpango takribani kaya 173,076 baada ya kuhitimu ifikapo Januari 2023.

"Kaya hizo ni pamoja na kaya 156,586 zinazoondolewa kutokana na kuimarisha kiuchumi na kuweza kujitegemea bila ruzuku na kaya ya walengwa 16,490 ambazo zinapokea ruzuku ya uzalishaji," alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na utaratibu wa kuziondoa kaya ambazo zimetoka kwenye umaskini uliokithiri na kuimarika kiuchumi kuwa endelevu, kundi la pili la kaya 223,418 ambazo zimeimarika kiuchumi zinatarajiwa kuondolewa ifikapo Septemba 2023.

"Katika mpango wetu, tuna kaya zaidi ya 200,000 ambazo zinatarajia kuingia katika mpango wetu, ndiyo maana tumefanya tathmini walioimarika ili watoke wapishe na wengine waweze kuingia," alisema.

Aliongeza kuwa hatua ya kufanya mchakato wa kaya zilizoachwa ni katika kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuwarudia ambao wameachwa na mpango kwa sababu moja au nyingine.

"Awamu ya kwanza tulifikia asilimia 70 ya vijiji, mitaa na shehia, awamu ya pili tukamalizia asilimia 30, lakini bado kuna wengine ambao wamesahaurika na Rais Samia ameagiza tuwarudie wote walioachwa ili nao waingine na tunatarajia kaya zaidi ya 200,000 zitaingia baada ya hawa kuondolewa na hili zoezi ni endelevu," alisema.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Moleti wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma wakitengeneza makingamaji kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo mashambani, wanafunzi hao wamepatiwa mafunzo kupitia mradi wa kuwezesha jamii yenye ustahimilivu na ustawi kwa njia shirikishi za kilimo-ikolojia katika Nyanda kame. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakulima wa zabibu walia kwa kupata hasara

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

WAKULIMA wa zabibu wilayani Chamwino mkoani Dodoma wameiomba Wizara ya Kilimo kuharakisha utekelezaji wa ujenzi wa viwanda vitatu vya kusindika mvinyo ghafi ili kuwaepusha na hasara kubwa ambayo wamekuwa wakiipata kila mwaka.

Katika mwaka huu wa fedha (2022/23), serikali imetoa Sh. bilioni tatu kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa viwanda vitatu vya kusindika mvinyo ghafi kwenye maeneo la shamba la zabibu la Chinangali II, Mpunguzi na Hombolo kwa ajili ya kuongeza wigo wa soko la zabibu.

Pia katika miaka karibuni, wakulima wa zabibu za mvinyo wamekuwa wakikabiliwa na kero kubwa ya uhaba wa soko la uhakika, hali ambayo ililazimu serikali kuja na mpango wa kujenga viwanda hivyo ili kutanua wigo wa soko la zabibu hizo.

"Baada ya serikali kutangaza ujenzi wa viwanda hivyo, wakulima wengi mkoani Dodoma walihamasika kuanza kulima zabibu za mvinyo kutokana na matarajio ya kupata soko la uhakika kwenye viwanda hivyo.

"Hata hivyo, tunashindwa kufahamu kwanini mpaka sasa ujenzi wa viwanda hivyo haujaanza wakati serikali imetoa fedha kwa Wizara ya Kilimo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo," alisema David Mwaka, Mwenyekiti wa Umoja wa Wakulima wa Zabibu Tanzania.

Alisema kuwa kwenye shamba la Chinangali II pekee, wakulima tayari wamepanda zaidi ya ekari 600 za zabibu za mvinyo kwa matarajio makubwa kwamba soko la uhakika litapatikana kutokana na ujenzi wa kiwanda katika shamba hilo kubwa la zabibu nchini. "Msimu wa mavuno unatarajiwa kuanza mwezi Septemba mwakani na endapo wizara itakuwa haijajenga viwanda hivyo, wakulima wataingia hasara kubwa sana ya zabibu kuozea mashambani kama ilivyotokea katika msimu uliopita," alisema. Alikumbusha kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa amefanya jitihada kubwa katika kuboresha kilimo cha zabibu na kuchochea sekta ya viwanda vya mvinyo, hatua ambazo zitakuwa hazijazaa matunda kama Wizara ya Kilimo itashindwa kujenga viwanda hivyo kwa wakati unaotakiwa.Mwenyekiti huyo aliongeza kuwa wamefanya jitihada kadhaa za kuwasiliana na wizara husika ili kujua mchakato wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa viwanda lakini hawajapata majibu yanayoridhisha.

"Kwa mujibu wa taarifa tulizopewa na Wizara ya Kilimo, mchakato unaendelea kumpata mkandarasi ambaye atatekeleza ujenzi wa viwanda hivyo katika viwango vinavyotakiwa, lakini hofu yetu ni muda, kama ujenzi hautamalizika kwa wakati, zabibu zetu zitaozea mashambani," alisisitiza.

Tanzania inashika nafasi ya pili baada ya Afrika Kusini kwa kutengeneza mvinyo bora zaidi barani Afrika na nchi ina uwezo wa kufanya vyema zaidi kutokana na kuwa na hali ya hewa nzuri inayowezesha zabibu kuvunwa kwa misimu miwili kwa mwaka, hali ya hewa ambayo haipo katika eneo lingine duniani.





# 'Jiandaeni kwa mitaala mipya ya elimu nchini'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imewataka wadau wa sekta ya elimu kujiweka tayari kwa matumizi ya mitaala mipya ya masomo ya msingi na maandalizi inayotarajiwa kuanza kutumika mwakani.

Waziri wake, Lela Muhamed Mussa alitoa kauli hiyo jana wizarani kwake Mazizini Zanzibar alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu matumizi ya mitaala mipya ya elimu baada ya kufanyika marekebisho makubwa.

Alisema mitaala mipya ya elimu inayotarajiwa kutumika mwakani, imezingatia mahitaji ya elimu kwa wanafunzi kwenye mazingira tofauti, elimu ya vitendo ikipewa kipaumbele zaidi.

Alisema marekebisho hayo yamefanyika baada ya kujitokeza changamoto mbalimbali ikiwamo ufaulu usioridhisha kwa wanafunzi katika mitihani ya taifa ya kidatu ya nne.

"Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inapenda kuwajulisha wadau wake katika sekta ya elimu ikiwamo shule binafsi kwamba mitaala mipya ya elimu inatarajiwa kutumika mwakani ambayo inakwenda na mahitaji ya elimu yaliyopo sasa kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi kuwa na ufaulu mzuri," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Mwakheri Adam Ameir alisema mahitaji ya mitaala mipya ya elimu yamezingatia mahitaji ya elimu mjumuisho pamoja na upatikanaji wa vifaa vyake ikiwamo kuwapo shule zenye mahitaji hayo.

"Tumejipanga kuhakikisha tunaingia katika soko la ajira kwa mafanikio makubwa, mabadiliko ya mitaala ya elimu yamelenga kuimarisha elimu mjumuisho pamoja na kuwapo shule zenye mahitaji hayo," alisema.

# Chanzo cha kifo ndugu wa Bakhresa chaishtua serikali

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman amewataka watendaji kubadilika na kuchukua hatua za ziada katika kupambana na uhalifu unaojitokeza kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Othman aliyasema hayo alipofika kuifariji familia ya mfanyabiashara maarufu nchini, Said Salim Bakharesa kufuatia kifo cha mwanafamilia Salim Ahmed Salim Bakharesa aliyevamiwa na kujeruhiwa kwa visu na watu wasiojulikana na baadaye kufariki dunia akiwa hopitalini nchini Afrika ya Kusini alikopelekwa kwa matibabu.

Othman alisema watendaji wa vyombo mbalimbali hawana budi kutambua kwamba Mji wa Zanzibar umekuwa na tabia na mienendo isiyofaa, hivyo lazima wachukue hatua sahihi na za ziada kutokana na mabadiliko hayo.

Alisema uhalifu unaojitokeza kwenye maeneo mbalimbali unatokana na kubadilika kwa tabia za wanajamii sambamba na kuongezeka watu wenye hulka tofauti, jambo linalochangia kujitokeza vitendo vingi vya uhalifu.

Alisema wanajamii na wasimamizi wa sheria nchini watakiwa kuwa na mtazamo mwingine na kubadilika katika utendaji wa kazi zao na kuyatazama masuala ya kiutendaji kwa upana zaidi kuliko ilivyo sasa ili kukabiliana nayo kwa usahihi na uhakika.

Alisema tabia mseto zinazojitokeza Zanzibar zinachangia kuwapo matukio ya aina mbalimbali ya uhalifu, jambo linalohitaji watendaji kufanya kazi ya ziada katika kupambana na hali hiyo isiendelee nchini.

Makamu wa Rais alisema jamii na vyombo vya kiutendaji vinahitaji kufanya marekebisho ya utendaji wao ili kuwa na mbinu bora na za kisasa katika kukabiliana na uhalifu wa aina mbalimbali nchini.

Alisema licha ya serikali kujitahidi kuweka mikakati imara katika kupambana na masuala ya uhalifu na hasa udhalilishaji, masuala hayo yamekuwa yakiongezeka kutokana na mji kukua na idadi ya watu kuongezeka na kwamba mabadiliko ya kiutendaji ni jambo linalohitajika kwenye maeneo yote.

Mwanafamilia hiyo Ahmed Salim Bakharesa alisema kuna haja serikali kufikiria kuweka mkazo na kulipa nguvu zaidi Jeshi la Polisi na kuihusisha jamii ili isaidie vyema katika kukabiliana na vitendo vya uhalifu nchini.

Salim Ahmed Salim Bakharesa aliyevamiwa na watu wasiojulikana nyumbani kwake na kujeruhiwa kwa kisu wiki chache zilizopita, alipelekwa kwenye Hospitali ya Hill Park mjini Johannesburg, Afrika Kusini ambako alifariki dunia na kuzikwa juzi.



Makamu wa kwanza wa Rais Zanzibar, Othaman Masoud akisalimiana na mfanyabiasha Said Salim Bakharesa baada ya kufika katika familia hiyo mjini Zanzibar kuwafariji kufuatia kifo cha mtoto wao Salim Ahmed Bakharesa kilichotokea hivi karibuni **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Waziri ajivunia kukamilika kwa Sera Uchumi wa Bluu na Uvuvi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Masoud Suleiman Makame amesema kukamilika kwa Sera ya Uchumi wa Bluu pamoja na Sera ya Uvuvi ndani ya kipindi cha mwaka mmoja wa 2022 ni hatua kubwa ya maendeleo.

Amesema sera hizo ni bora na zenye kuleta matumaini kwa wananchi wa Zanzibar.

Aliyasema hayo jana wakati wa semina ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu uelewa wa rasimu za sheria mpya za uvuvi na mazao ya baharini, uhifadhi na utafiti wa uvuvi na rasilimali zake iliyofanyika mjini Unguja.

Alisema kuwa kutokana na kukamilika kwa Sera ya Uvuvi Zanzibar, wizara yake imekamilisha rasimu za sheria ya maendeleo ya uvuvi, sheria ya uhifadhi wa rasilimali ya bahari na sheria ya utafiti wa maliasili za bahari.

"Nikiri kwamba wavuvi wenyewe wamepata fursa ya kutoa maoni yao kuhusu sheria hizo kwa Unguja na Pemba," alisema.

Waziri huyo alisema sera na rasimu ya sheria tatu zilizotayarishwa na watendaji wa wizara hiyo zimezingatia mahitaji ya wavuvi na jinsi ya kuwaendeleza wavuvi na wafugaji wa mazao ya baharini.

Alisema sera na sheria hizo zimeangalia uzoefu wa nchi za visiwa na kuzingatia maendeleo ya sekta ya uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini.

Akifungua semina hiyo, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma alisema serikali imefanya uamuzi sahihi kwa lengo la kukuza uchumi wake kupitia rasilimali ya bahari.

Alisema amefarajika kuona Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi imeandaa sera na sheria ya uvuvi ikiwashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wavuvi na wadau wengine ili kupata mwongozo mzuri.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema wizara hiyo ina wigo mpana wa maendeleo na hivi sasa uvunaji wa samaki umefikia tani 55,000 visiwani Zanzibar.

Alisema wizara inafanya kazi kubwa ya kuwafundisha wavuvi wadogo waliopewa boti za uvuvi kuhusu matumizi ya vitafuta samaki (fish finder) na mwelekeo wa kuwaongoza wavuvi baharini (GPS) ili wavuvi kufanya kazi zao kwa ufanisi, uhakika na kisasa zaidi.



**NATURE**
UKURASA 16

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI DESEMBA 31, 2022




# MAMA TOTOO

YUKO WAPI ?

# MUHIDIN GURUMO-1

# Sauti ya radi inayounguruma, muasisi majina Msondo, Sikinde



**Na Adam Fungamwango**

BENDI kongwe za muziki wa dansi nchini Msondo Ngoma, na Mlimani Park Orchestra ni mahasimu kwenye muziki huo na hufananishwa kama vile zilivyo klabu za Simba na Yanga kwenye soka.

Bendi hizi zina mashabiki wengi kila pande na huwa wanabishana, kugombana mpaka kupigana huko mitaani na vijiweni.

Kwa sasa hata kwenye mitandao ya kijamii, mashabiki wa bendi hizi wamekuwa wakishindana na kubishana kila moja akidai nyimbo za bendi yao ni bora zaidi kuliko wapinzani wao.

Lakini si wengi wanajua kuwa majina ya mitindo ya bendi hizo ndiyo yanayozitambulisha zaidi, yameasisiwa na mtu mmoja tu.

Aliyeasisi jina la Msondo Ngoma, ndiyo huyo huyo aliyeasisi jina la Sikinde Ngoma ya Ukae. Hii yote ni mitindo ya bendi hizo.

Ni kama vile awe mtu ambaye huyo huyo ndiye aliyebuni jina la Yanga, halafu aende tena kwenye klabu ya wapinzani akabuni jina la Simba na majina yote yakakubalika na kutumiwa hadi leo hii. Huyu si mwingine bali ni mwanamuziki nyota kabisa kuwahi kutokea kwenye ardhi ya Tanzania, Muhidini Mwalimu Gurumo.

Ndiyo, hilo ni jina lake halisi, japo kuna watu wanamwita Muhidini Maalim Gurumo.

Huyu ni mwanamuziki mwenye karama ya uongozi, aliyezaliwa mwaka 1940 kijiji cha Masaki, Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani.

Alifariki jijini Dar es Salaam Aprili 13, 2014 akiwa na miaka 74 kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa ugonjwa wa moyo.

Historia inaonyesha kuwa, kila anapokwenda anabuni jina la mtindo wa bendi ambalo linashika na kuwa maarufu kwa wapenzi na mashabiki wa muziki wa dansi.

Mbali na kuwa na karama ya uongozi ni mwimbaji na mtunzi ambaye alianza kuimba sauti ya kwanza, lakini kadri muda ulivyozidi kwenda na kupokea wanamuziki wengine vijana, alirudi na kuanza kuimba sauti ya pili na ya tatu, huku yeye akiimbisha.

Kwenye makala hii tunamzungumzia mwanamuziki huyo tangu kuzaliwa kwake, nini kilimsukuma kwenye muziki, alivyoanza, changamoto, kilele cha mafanikio, jinsi alivyoasisi majina ya mitindo ya bendi hizo, uongozi wake na hata kifo chake.

**Kuzaliwa kwake, changamoto ya jicho**

Kama nilivyoandika awali kuwa alizaliwa kwenye Kijiji cha Masaki Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani na elimu yake ya msingi alisoma katika Shule ya Pugu kuanzia darasa la kwanza mpaka la tatu, 1956 mjomba wake aliamua kumuhamishia Dar es Salaam ambako alisoma zaidi elimu ya dini, Mtaa wa Lindi, Ilala, Dar es Salaam.

Kila kitu kina sababu, huenda asingekwenda Dar es Salaam asingeweza kuwa mwanamuziki maarufu ambapo leo hii ni miaka minane bado anaendekea kukumbukwa.

Kwa mujibu wake mwenyewe wakati wa uhai alisema changamoto ya jicho iliyompata ilitokana na kuangukiwa na jiti akiwa na wiki chache tu tangu azaliwe.

"Nyumbani kwetu kuna miembe mingi, nililazwa chini ya mwembe, unajua watoto wachanga huwa wanalazwa chali na mama zao kwenye kivuli, nadhani ilikuwa wiki tatu au mwezi hivi tangu nizaliwe, likadondoka jiti la mwembe likaja kunipiga jichoni," alisema Gurumo wakati wa uhai wake.

Kuanza kwake muziki rasmi

Mara nyingi Gurumo anapozungumza, historia yake inaanzia NUTA Jazz, lakini ukweli ni kwamba alianza muziki mwaka 1960 akiwa na miaka 20 tu kwenye bendi ya Kilimanjaro Chacha.

Mwenyewe alisema, alirithi muziki kutoka kwa mama yake ambaye alikuwa akiimba kwenye vikundi vya ngoma za asili ya kizaramo.

"Mimi kuimba nilirithishwa na mama yangu, alikuwa anaimba kwenye vikundi vya ngoma ya asili ya kizaramo inayoitwa 'Ndekule', wakati huo bado msichana," alisema mzee Gurumo wakati wa uhai wake.

Itakumbukwa kuwa alipoihama Sikinde mwaka 1985 na kwenda kujiunga na Orchestra Safari Sound ambayo ilikuwa imeondokewa na mwanamuziki Freddie Ndala Kasheba na mtindo wake wa 'Dukuduku', Gurumo aliuondoa mtindo huo na kuasisi mtindo wa 'Ndekule.'

Kumbe ilikuwa ni jina la ngoma ya kikundi cha asili ambacho mama yake alikuwa akiimbia.

Hakukaa sana na bendi ya Kilimanjaro Chacha kwani miaka miwili baadaye 1962, akajiunga na Rufiji Jazz Band, nako pia ni kama alitia pua tu, mwaka mmoja baadaye akaenda bendi ya Kilwa Jazz.

Mwaka 1964 alikuwa mmoja kati ya waasisi wa bendi ya NUTA Jazz ambayo ilibuni mtindo wake wa 'Kiwelewele'.

Bendi hii ilikuwa inamilikiwa na Chama cha Wafanyakazi na ilikuwa inabadili majina yake kutokana na mabadiliko ya siasa na mfumo wa uendeshaji.

**Inaendelea wiki ijayo.....**

## UDAKU TU




# WANAMTAKA BABA
## Mama Totoo aambiwa

MKUU wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, hatimaye amefunga mwaka kwa kupata zawadi kubwa katika maisha yake, baada ya kujifungua mtoto wa kike.

Mrembo huyo ambaye ameingia katika uongozi wa kisiasa, awali alikuwa mshiriki wa shindano la Miss Tanzania na mpambaji wa video za muziki wa Bongo Fleva, amejiunga katika orodha ya mastaa wa kike waliofanikiwa kuwa na watoto hivi karibuni.

Tayari Jokate amemtambulisha mtoto wake ambaye amependekeza kuitwa Totoo na yeye kuwa Mama Totoo.

Mastaa mbalimbali wa nje na ndani ya nchi wamejitokeza kumpongeza kwa kupata mtoto na kumtakia maisha na malezi mema.

Hata hivyo, swali la baba wa mtoto huyo limebaki kuwa kitendawili, licha ya fununu kuwepo kuwa mfanyabiashara maarufu Fredy Funjabei ndiye baba halisi wa Totoo.

Vunjabei kwa upande wake licha ya kumpongeza Jokate, aliandika ujumbe wa kipekee kutoka kwenye kitabu cha Biblia wa kumkaribisha mtoto huyo.

"Kabla sijakuumba katika tumbo, nilikujua na kabla hujatoka tumboni nilikutakasa, nimekuweka kuwa nabii wa mataifa," Jeremia 1:5

Mwegelo ambaye alijifungua wiki chache zilizopita alipakia picha akiwa amempakata mtoto wake mchanga mikononi huku akiwa amejawa na furaha na kuwaomba mashabiki zake kumuita mama Totoo.

Mwegelo ambaye anakubalika na mashabiki zake kwa utendajikazi wake, bado amekuwa gumzo kutokana na ukimya wake wa kumtaja baba wa mtoto huyo ambaye tangu alipotambulishwa amekuwa maarufu.

Baadhi ya mashabiki walimtaka Jokate na Vunjabei kutamka bayana kuwa sasa ni wazazi na pengine kuweka wazi mipango yao ya maisha ikiwamo kufunga pingu ya maisha.

"Jokate ni mpambanaji, mchapakazi na mbunifu katika majukumu yake, lakini kukaa kimya kuhusu baba wa mtoto kunaweza kuwachanganya watu," amesema Halima Sikunjema.

Jokate aliyekuwa mfanyabiashara na mtangazaji, aliteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe mnamo mwaka 2018, kisha 2017 alitajwa kwenye orodha ya Forbes kuwa miongoni mwa wanawake 30 bora wenye chini ya miaka 30.

BASI SAWA

## Sholo Mwamba ampa tano Dulla Makabilla



Msanii wa muziki wa singeli, Sholo Mwamba amempigia saluti mwenzake Dulla Makabila kwa dude lake ambalo kwa sasa ni habari ya mjini 'Pita Huku'.

Sholo, mmoja wa wasanii waliofanya mapinduzi makubwa kwenye muziki wa singeli amempata Dulla ili kuangalia serikali kupitia BASATA inasema nini ili kurekebisha kasoro zilizopo.

"Namfahamu Dulla na najua hisia zake, kuna maneno mle kaimba kwa hisia zake. Ni mtu wa hivyo na anayependa utani, ile kumuimba Lavalava pia ni mambo yale yale ya utani kwa sababu hata mimi ameshawahi kuniimba kuwa niache muziki niende kufuga mbwa, yaani yeye ni mtu wa hivyo. Mimi namsapoti kwa sababu nami pia ni msanii wa singeli, tunataka muziki wetu ukae juu," alisema Sholo.

Msanii huyo alisema hayo kufuatia wimbo wa 'Pita Huku' wa Dulla Makabila ambao ameutoa hivi karibuni kuibua hisia tofauti kutoka kwa watu tofauti kiasi cha kuitwa na Baraza la Sanaa Basata.

## Rais wa Kitaa awapa darasa wasanii



Msanii aliyejizolea mashabiki wengi kwa sasa, 'Nay wa Mitego' amewataka wasanii wenzake kuwa na tabia ya kupuuzia vitu vidogo vidogo alivyoviita vya kijinga kwa kulaumu kutokuwa kwenye orodha ya wasanii bora ambayo imewekwa kimkakati.

Nay aliandika hayo baada ya baadhi ya wasanii kutowekwa kwenye orodha ya wasanii bora iliyotolewa na watu mbalimbali kwa siku za karibuni, huku baadhi ya wasanii walioonekana kufanya vema mwaka huu kutokuwepo kwenye orodha.

"Hivi msanii unaanzaje kulaumu kutokuwepo kwenye Top Ten ya mtu? Mwenyewe ana wasanii wake kawaweka juu kwenye hiyo chati na dunia inajua hawajafanya vizuri, unaanzaje kulalamika? Jifunzeni kupuuza ujinga ndugu wasanii. Wananchi wanajua nani kafanya vizuri huu mwaka," aliandika Nay kwenye mtandao wa kijamii.

Hivi karibuni baadhi ya watu maarufu wamekuwa wakitoa Top Ten zao ambazo zimekuwa zikikosolewa na baadhi ya wasanii kwa madai hazijawatendea haki wengine kwa kutokuwaweka.



## JUMA NATURE HANA MBAMBAMBA 2023

Msanii mkongwe wa Hip Hop Juma Nature ameamua kuacha kazi na kufanya kazi mwaka 2023, kwani ameingia studio akitengeneza dyde ambalo anatarajia kuliachia hivi karibuni.

Ngoma hiyo imeanza kusubiriwa kwa hamu na mashabiki wake ambao wamemmisi kinoma, itakuwa ni ya kwanza kwake kwa mwaka 2023.

Mwenyewe amefunguka, anadai yuko studio. Anaandaa kitu cha uhakika kwa mashabiki zake ambao wanadai, hajawahi kukosea hata siku moja.

"Studio napika chombo kambini kaeni mkao wa kula haina mbambamba," aliandika kwenye mtandao wake wa instagram huku akiwa ameweka picha yake, akiwa anaandika mistari na pembeni yake akiwa ameketi mtayarishaji wake wa muziki maarufu kama 'prodyuza'.

Baadhi ya mashabiki zake wakamjibu kuwa wanaisubiri kwa hamu. "Yupo mkaoni tunaisubiri," aliandika shabiki wake moja na mwingine akaandika, "Najua Kassim Kiroboto huna shoo mbovu."





## Luiza ataja wezi wa kazi ya muziki

Mwenyekiti wa Chama cha Muziki wa Dansi Tanzania (CHAMUDATA), Luiza Mbutu amesema kwa sasa wezi wa kazi za muziki wako kwenye mitandao ya kijamii, ambapo wamekuwa wakiiba kazi za wanamuziki na kuziuza kwa kupitia njia hizo.

Luiza ambaye pia ni kiongozi wa bendi ya African Stars "Twanga Pepeta' amesema baadhi ya waliokuwa wakiiba kazi zao wamewakamata, wakakiri na kuwalipa, kwa sasa wanafanya nao kazi ingawa baadhi yao wapo nje ya nchi hivyo inakuwa ngumu kuwapata.

"Mnatoa albamu ya nyimbo sita au saba, unakuta zile nyimbo zimeshawekwa kwenye mitandao ya kijamii, halafu mtunzi mwenyewe ukitaka kuweka inakukatalia, kwa sababu kuna mtu ameshaingiza, hii inatupa tabu sana mpaka kuja kuwapata, lakini tunajitahidi sana, wengine tunawapata, wengine wapo nje ya nchi," alisema mwanamuziki huyo.

## 'WAMETRENDI' MWISHONI 2022

**Na Adam Fungamwango**

LEO ndiyo mwisho wa mwaka 2022 ambao unaisha na mambo mazito. Ulionekana utamalizika kama kawaida, lakini imekuwa sivyo. Kuna mambo yamejitokea hapa mwishoni mwa mwezi Desemba kiasi kwamba mwaka umeisha kwa mshikemshike usio wa kawaida.

Hebu tuangalia ni akina nani ambao wamefanya mwaka huu umalizike kwa kishindo na kuzua mijadala mbalimbali.

**Dulla Makabila**



Msanii aliyetrendi sana mwishoni mwa mwaka huu ni mwimbaji wa nyimbo za singeli, Dulla Makabila. Kilichomfanya azungumzwe kila kona ni wimbo wake wa 'Pita Huku'.

Ni wimbo aliouachia kwenye mtandao wake wa kijamii Desemba 19 na kuwa gumzo kila kona. Tayari zaidi ya watu milioni moja na nusu wameutazama wimbo huo kupitia mtandao wake wa instagram. Ni wimbo ambao kwa ufupi maudhui yake yanaonyesha kuwa wanayoyaona binadamu inawezekana ikawa tofauti kwa Mwenyezi Mungu. Mtu anaweza kuonekana hana hadhi yoyote kwenye jamii, lakini kumbe alikuwa akifanya mema hivyo akaenda peponi na wale ambao machoni mwa watu walionekana wema, kumbe sirini ni wachafu wakaenda motoni kwa sababu Mungu anaona kile ambacho bindamu haoni.

Hata hivyo, baadhi ya maneno yake yameleta matatatizo, na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kumtaka aondoe baadhi ya maneno kwenye wimbo huo.

**Diamond Platnumz**

Kuugua kwa msanii nyota kabisa nchini Tanzania na Afrika kwa ujumla, Abdul Naseeb, maarufu kama Diamond Platnumz kulizua gumzo na taharuki si kwa mashabiki zake tu, bali kwa muziki wa bongo fleva kwa ujumla.

Kwenye video alizozishea mwenyewe kwenye ukurasa wake wa instagram, akieleza hayo kuwa mwaka huu haukuwa mzuri kwake kwenye sikukuu hii ya Noeli kwani amesherehekea akiwa kitandani.

**Sallam SK**

Mwingine ni meneja wa msanii Diamond Platnumz, Sallam SK ambaye ametrendi sana baada ya kutoa maoni yake kuhusu wasanii waliotamba mwaka huu na kuzusha mjadala mkubwa kwenye mitandao ya kijamii.

Akatoa 10 bora ya wasanii hao ambao aliwaweka kwenye namba, ambapo Diamomd Platnumz alishika namba moja, huku Zuchu akiwekwa namba mbili.

Mbosso, kwa mujibu wa meneja huyo ameshika nafasi ya tatu na ya nne ilikwenda kwa Marioo, Rayvanny akiwa kwenye namba tano.

Msanii Jay Melody aliwekwa kwenye namba sita, msanii mkongwe Ali Kiba alitupwa namba saba, Nandy namba nane, nafasi ya tisa ikamwendea Lavalava na Harmonize akapewa namba 10.

**Harmonize**

Mara baada ya meneja huyo kutoa orodha hiyo kulingana na maoni yake, msanii Harmonize, licha ya kuwekwa namba 10, alijitokeza na kumpongeza Sallam SK sana kupitia insta stori yake, akidai namba hiyo 10 kwake anaifananisha na mchezaji wa taifa ya Argentina, Lionel Messi. Hiyo nayo ikazua mjadala mkubwa na kumfanya atrendi.

**Ali Kiba**

Naye ameingia kwenye orodha ya waliotrendi baada ya kuwazodoa wote ambao aliodai wanatengeneza orodha za wasanii kimkakati na kwa sababu wanazozijua wenyewe.

FILAMU

## Mfaume:Penzi halinunuliwi kama pipi

**Na Adam Fungamwango**

KUNA mnyukano wa kimawazo kwa wale wanaodai kuwa mapenzi ni pesa, na wale ambao wanakataa hilo. Inawezekana wote wakawa wako sawa, lakini wanachoshindwa kuweka sawa pale ni kitu gani kinaanza.

Pesa ikianza ndiyo yakaja mapenzi hapo hakuna kitu. Kinachotakiwa hapo mapenzi yaanze, halafu pesa ifuatie. Wengi wanakubaliana kuwa pesa ni mbolea kwenye mapenzi. Lakini kinachotakiwa kwanza mapenzi yaanze. Lakini ikiwa mapenzi hayo msingi wake ni pesa hayatadumu kamwe.

Wito kwa wanaume ni kwamba huwezi kumnunua mwanamke kwa pesa. Utakachonunua labda ni huduma yake ya muda, lakini si moyo wake. Mapenzi ya binadamu yapo kwenye moyo na msingi wake ni hisia na upendo.

Tuiangalie filamu iitwayo 'Mfaume' iliyochezwa na Ramadhani Wawa, Dunia Kiamba, Hamisi Sozigwa, Scolla Victor, Tahiya Mussa na wengine wengi.

Sam anaishi vema na mkewe Faraja ingawa hali yake na kipato ni duni. Mkewe hajui kazi ya mumewe, lakini anachojua ni kwamba mumewe anatoka kwenda kutafuta, lakini hali yao ni ya chini.

Siku moja yupo na shoga zake mbali na maeneo ya nyumbni, anamuona mumewe anaokota chupa na kubeba taka za watu kwenda kumwaga, hiyo ndiyo kazi yake. Shoga zake wanamwambia hiyo ndiyo kazi ya mumewe miaka yote.

Baada ya tukio hilo alililoliona ni kama mapenzi yalianza kupungua kwa mumewe na akaanza kumfanyia vituko. Faraja ni mwanamke mrembo, ila hali duni ya mumewe ndiyo inayomfanya aonakane amefujika.

Kuna jamaa mmoja mwenye pesa zake anaitwa Sam, akamtongoza mke wa Mfaume. Mapenzi yakaanza kuwa motomoto hadi mwenyewe akatambua. Akamfuata na kwenda kumuonya kuwa aache kutembea na mkewe kwa sababu si jambo la kiungwana. Anaambulia dharau kutokana na ufukara wake.

Hatimaye, Sam anamwambia Faraja kuwa amuache mumewe kwa sababu hawezi kushea na mwanaume muokota makopo.

Faraja anafanya kama alivyoambiwa na hawara wake. Kabla ya kuondoka 'anamnanga mumewe' aliyekuwa analia kutokana na kuachwa.

"Acha uchukuro, haya maisha yako uliyoamua kuishi kwenye kijumba chako na kitanda chako cha kamba yamenichosha, siyawezi, naenda zangu huko kwa wenzako wanaojua kulea, naenda kula vinono. Lo! masikini, unasikitisha. We unadhani nitalala kwenye kitanda cha kamba hadi lini? Mimi maisha haya siyawezi, naenda kula vitamu, kulalia vitanda vizuri, huko naenda kulelewa kama malaika, siyo huku kila siku mlenda na matembele."



Akili za kuambiwa changanya na zako. Sam anambadilikia na kumtimua. Anamwambia kama amekubali kumkimbia mumewe na yeye pia ipo siku akikutana na mwenye pesa zaidi yake atamkimbia.

Faraja hana pa kwenda. Akaenda kuishi kwa shoga yake na maisha ya 'kudanga'. Maisha yanamchosha, akarejea kwa mumewe kuomba msamaha. Mumewe anamsamehe, anakopa pesa na kumpa msingi wa kuuza mkaa. Maisha yanaendelea na yanakuwa afadhali kuliko ya mwanzo.

mwisho

BONGO FLEVA

# HAJITOI MTU HAPA



MMOJA wa mameneja katika lebo ya Wasafi, Saidi Fella, maarufu kama Mkubwa Fella, amekanusha uwepo wa mgogoro wa uongozi katika kundi hilo, na kwamba kinachozungumzwa na watu hakuna ukweli wowote.

Hivi karibuni kumeibuka mjadala mkali baada ya uvumi kuibuka kwamba mmoja wa meneja wa lebo hiyo, Sallam Sk, amejitoa kufuatia kuwa na tofauti na mwanamuziki Diamond Platnumz.

Hata hivyo, minong'ono hiyo iliisha baada ya Sallam Sk kutoa orodha yake ya wanamuziki waliofanya vizuri. Wanamuziki walio chini ya wasafi akiwaweka katika namba za juu mwanzoni.

Akizungumza kupitia redio ya Wasafi, Fella amesema hakuna hata meneja mmoja kati ya watatu waliojitoa katika lebo hiyo, na kueleza kwamba ukimya wao haukuashiria mabaya bali ni neema.

"Haya maneno yanatoka wapi? Hakuna aliyejitoa wasafi, sisi sote bado tupo na tunaendelea kutimiza majukumu yetu kama kawaida," amesema Fella.

Amesema, kuambatana na wasanii kila kona ni alama ya utendaji wa kazi, bali kuna wakati watu wanafanya kazi kimya kimya bila kuonekana kwa kutumia njia za kisasa.

"Tuna kundi la Whatsap linaloitwa Viongozi Wakuu, huko ndiko tunazungumza na kufanya kazi, haya masuala ya kuonekana mara huku na Diamond mara kule yamepitwa na wakati. Wanatakiwa kuamini kila kitu kiko sawa," ameongeza kusema.

Akizungumzia ujio wa kibao kipya cha Diamond kinachoitwa 'Chitaki', amesema hiyo ni kazi yake mwenyewe kwa asilimia 100 na hakuna mtu aliyeingiza mkono wake.

Fella, amesema kwa kawaida Diamond anapotunga wimbo unapitia katika mikono ya viongozi wote kuangalia maudhui na maneno kama yanaweza kuuza, lakini safari hii wameamua kumpa uhuru wa kutunga na kuachia muziki bila wao kurekebisha.

"Huu wimbo Chitaki ni wake mwenyewe, hakuna mtu aliyeingiza mkono wake tumemwambia haya utambulishe tuangalie kama utawashika wasikilizaji. Lakini mapokeo yake yanafurahisha sana kwa kila kona umeshika vibaya,"amesema.



## BATA LA WIKI

**Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368**

**Dar Musica Original**

Bendi hii inayoongozwa na Jado Field Force, leo mkesha wa Mwaka Mpya, itafanya vitu vyake kwenye Family Part ndani ya Bwalo Kuu la Magereza Ukonga ikitambulisha nyimbo za 'Dance Powerfull na Yatima Hadeki'.

**Kimokimo Band**

Wakiwa chini ya Khadija Mnoga 'Kimobitel', leo mkesho wa Mwaka Mpya wapo ndani ya ukumbi wa Royal Garcden Kijichi, kesho sikukuu ya Mwaka Mpya watafanya vitu vyao katika ukumbi wa D Pub Mbezi Msumi.

**Waluguru Original**

Kama kawaida yao leo Jumamosi wapo ndani ya ukumbi wa Terminal Pub Msamvu, mjini Morogoro, kesho siku sikukuu ya Mwaka Mpya, watatoa burudani katika ukumbi wa F2 Florida.

**Orchestra Sikinde Original**

Baada ya kumaliza sikukuu ya Krismasi, kesho siku ya Mwaka Mpya watafanya vitu vyao katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**Town Classic Band**

Bendi hii mpya kabisa, leo Jumamosi watafanya makamuzi ya nguvu katika ukumbi wa Kisuma Bar Magomeni, kesho sikukuu ya Mwaka Mpya wataibukia katika ukumbi wa Twist Lounge Tabata.

**FM Academia**

Leo Jumamosi mkesha wa Mwaka Mpya watakinukisha katika ukumbi wa Kibozone Malamba Mawili, kesho sikukuu ya Mwaka Mpya wapo ndani ya ukumbi wa Empire Sports Bagamoyo mkoani Pwani.

**Twanga Pepeta**

Baada ya kumaliza kukiwasha wakati wa sikukuu ya Krismasi, leo Jumamosi wapo ndani ya ukumbi wa Kiduli Garden Magomeni, Sikukuu ya Mwaka Mpya watakuwa ndani ya Andrews Lounge Sinza.



# AMALIZA NA KIBENTEN 2022

MASTAA wengi wanamaliza 2022 katika njia zao tofauti, wako wanaofurahia kupata mafanikio ya kazi zao na wengine kuongeza familia au mali.

Hata hivyo, Zari Hassan, ambaye ni mfanyabiashara na mama watoto wa mwanamuziki maarufu nchini Diamond Platnumz, yeye amekuwa tofauti kwani anamaliza mwaka akiwa na malalamiko ya kuvunja ndoa ya mtu.

Siku chache zilizopita mwanamke mmoja nchini Uganda anayeishi Marekani, amejitokeza huku akimshutumu Zari kwa kumuibia mume wake anayeitwa Shakib Cham Lutaaya.

Mwanamke huyo, Nalule Shamirah Sembatya, maarufu kama Mimi, amedai kuwa yeye ndiye mke halali wa Lutaaya na alithibitisha kwa kuchapisha cheti cha ndoa katika mitandao ya kijamii.

Kwa upande wa Zari ameonekana kutupilia mbali madai hayo akieleza malalamiko ya mwanamke huyo sawa na kutafuta kiki kupitia kwake.

Zari ambaye ni mama wa watoto watano alimjibu mfuasi wake aliyetaka kujua ukweli wa madai hayo ya kumchukua mume wa mtu kupitia Instagram. Akijibu kwa mkato, Zari alimwambia shabiki huyo kuwa huyo ni "Watafuta kiki."

Kulingana na cheti hicho ambacho Nalule alikitoa, inaonyesha yeye na Shakib walifunga ndoa mwezi Juni 2016.

Nalule pia alidai kwamba Mei 2017 alimpa Shakib visa ya kwenda Marekani kama mchumba wake, hivyo kumpa uwezo wa manufaa kadhaa.

Lakini hasa anamshutumu mwanaume huyo kwa kumkimbia na kwenda kwa Zari, licha ya kuwa na ndoa ya kisheria.

Kama haitoshi, Zari alipigilia msumari wa moto kwa kufichua kuwa tayari amepiga hatua ya kukutana na wazazi wa Shakib Lutaaya na kubainisha kuwa yuko tayari kupeleka mahusiano yao ya miezi kadhaa katika kiwango cha juu zaidi.

Mahusiano ya Zari Hassan na Shakib yamekuwa yakikosolewa sana hasa kwenye mitandao ya kijamii suala kuu likiwa ni utofauti wao wa umri. Zari ana umri wa miaka 42 wakati Shakib alitimiza miaka 31 hivi majuzi.

Mama huyo wa watoto watano hata hivyo alibainisha kuwa wazazi wa Shakib hawakuashiria tatizo lolote na mahusiano yao na kubainisha kuwa mkutano wao ulikuwa mzuri.

Chanzo: Jambo Radio

"Alinipeleka kuonana na wazazi wake na walikuwa wazuri sana, na sikumbuki hata kidogo wakilalamika kuhusu uhusiano huo," mzaliwa huyo wa Uganda alisema na kuongeza kuwa hatajitetea kabisa.

Zari pia alifichua kuwa anapanga kuongeza watoto zaidi na Shakib lakini akabainisha kuwa si kwa sababu ya shinikizo la umma.

# Zinoleesky kamaliza 2022 kicheko

MWIMBAJI wa Nigeria Zinoleesky, amemaliza mwaka kwa mafanikio ya hali ya juu baada ya kujiunga na orodha ndefu ya nyota wanaomiliki majumba mapya ya kifahari.

Mwanamuziki huyo alisambaza picha za nyumba yake kwenye mitandao ya kijamii huku akimshukuru Mungu kwa kumfikisha hatua hiyo. Alidai kuwa 2023 yake tayari imeanza.

"Asante bwana! 2023 yangu tayari imeanza," ameandika.





## Toyin hataki kuvunja nyumba

MWIGIZAJI na mtayarishaji wa filamu kutoka Nollywood, Toyin Abraham-Ajeyemi, amefichua kuwa hofu yake kuu ni kupoteza nyumba na ndoa yake.

Akishiriki katika kikao cha Media Room Hub, nyota huyo pia alijadili ndoa yake na kazi yake katika tasnia ya filamu.

Toyin alikiri kwamba wazo la kuishi bila mumewe ni ngumu, kuishi katika nyumba iliyovunjika imekuwa kama ni ndoto mbaya zaidi kwake.


## Nyota Ndogo kalewa kwa mzungu

MWANAMUZIKI mkongwe wa Kenya, Mwanaisha Abdallah, maarufu kama Nyota Ndogo amezidi kuwa sana mtandaoni kutokana na jinsi anavyojirusha na Mzungu wake wa Uholanzi Henning Nielsen.

Kulingana na machapisho yake kwenye mitandao ya kijamii ambayo yamekuwa yakisambaa, Nyota Ndogo amethibitisha kuwa anafurahia kuwa na mpenzi wake huyo mzungu.

Nyota Ndogo amejisifia kwamnba kuolewa na mwanaume ambaye amemzidi umri kumemfanya aonekane kama malkia na kuhisi kweli yuko kwenye mapenzi.





## Phyna hataki kujipandisha bega

MSHINDI wa Big Brother Naija, awamu ya saba Phyna, ametoa maoni yake kuhusu uzushi unavyoendesha tasnia ya burudani.

Nyota huyo ametoa maoni yake kupitia Snapchat, amedai kuwa watu wengi wanaishi maisha ya uwongo ili kujifanya kuwa matajiri na wazuri.

Amesema yeye hatashiriki katika udanganyifu kama huo, badala yake ataishi katika uhalisia.

## Tyler afa akila unga

MWIGIZAJI kijana wa Marekani, Tyler Sanders, amefariki dunia baada ya kudaiwa kuzidiwa na dawa za kulevya.

Nyota huyo wa filamu za 'Lone Star" na "Fear the Walking Dead," amekutwa akiwa amefariki ndani ya nyumba yake, huku kuna kila dalili kuwa kifo chake kilitokana na kuzidisha dawa.

Kulingana na ripoti hiyo, iliyopatikana na TMZ, Mkaguzi wa Matibabu wa jimbo la Los Angeles, pia amethibitisha kutokea kifo cha mtoto huyo wa miaka 18 na kueleza kilikuwa cha bahati mbaya.

Vyanzo vya uchunguzi wa kifo vilisema kuwa alikuwa na historia ya matumizi ya dawa za kulevya na polisi walipata majani ya plastiki na unga mweupe kwenye chumba alichofia.



MAKALA

# Ni miaka 13 tangu Simba wa Vita atutoke

## *Ni Rashidi Kawawa, rafiki wa Nyerere, alipenda kumwita Rashidi

Na Sabato Kasika

KWA kimo, alikuwa mfupi lakini pia mkakamavu, mchapakazi, si mwongeaji sana. Ukiona anatekeleza jambo, ujue ni uamuzi wa serikali.

Huyu si mwingine bali ni Rashidi Mfaume Kawawa ambaye leo anatimiza miaka 13 tangu afariki dunia.

Kila operesheni kubwa za Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Kwanza wa Tanganyika na baadaye Tanzania, alitekeleza yeye. Maazimio yote kuanzia mwaka 1967, miradi yote ya kitaifa, marufuku ya nguo fupi za wanawake, hata harakati za kuhamia katika vijiji vya ujamaa, alikuwa kinara katika utekelezaji.

Ni mmoja wa waanzilishi wa mgambo mwaka 1969 hadi anastaafu hakuwahi kuvurugana na Nyerere hadharani, wala hakuna rekodi yoyote ya kukwazana na aliwahi kuwa waziri asiye na wizara maalum.

Baada ya Tanganyika kuwa jamhuri mwaka 1962, aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu na hata baada ya Tanganyika na Zanzibar kuungana mwaka 1964 na kuwa Tanzania, alikuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais hadi mwaka 1977 alipoteuliwa kuwa Waziri wa Ulinzi akibadilishana na Edward Sokoine kuwa Waziri Mkuu.

Kwa ujumla, Nyerere alimwamini kupita kiasi na yeye akauheshimu huo uaminifu wake. Ndiye Katibu Mkuu wa Kwanza wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuanzia mwaka 1982, kabla ya hapo awali kulikuwa na cheo cha Katibu Mtendaji Mkuu.

Hata baada ya kifo cha Mwalimu Nyerere, aliendelea kulea taifa kuanzia serikali kama mlezi mkuu hadi kifo chake. Familia yake na ya Nyerere zimehamia kwenye undugu kwani pamoja na kazi, waliishi kindugu.

Alikuwa 'jembe' la Mwalimu katika serikali ya awamu ya kwanza, aliipenda TANU, CCM na matembezi ya mshikamano. Nyerere mwenyewe alipenda kumwita kwa jina la Rashidi. Alifariki dunia Desemba 31, 2009.



### KUVUTIWA NA NYERERE

Wakati yuko sekondari mkoani Tabora katika Shule ya Wavulana Tabora (wakati huo ikijulikana kama Tabora School), siku moja walikusanyika pamoja na wanafunzi wa shule zingine kwa ajili ya kujadiliana mada mbalimbali za masomo, huku baadhi ya wanafunzi wenzao wakiwa na walimu wao.

Miongoni mwa walimu hao ni Nyerere aliyemkosha Kawawa kutokana na alivyokuwa anafanyia maboresha mada walizokuwa wakijadili na kujenga hoja, hivyo kumfanya aendelee kumfuatilia, bila Nyerere mwenyewe kujua.

Baada ya kuhitimu masomo yake ya sekondari, aliajiriwa na kushiriki katika harakati za kutetea wafanyakazi. Kufikia mwaka 1955, alikuwa tayari Katibu Mkuu wa Shirikisho la Wafanyakazi Tanganyika (TFL).

Ndiye alikuwa kinara wa kuandaa migomo iliyotikisa serikali ya kikoloni hasa kwenye kampuni ya bia Dar es Salaam na Shirika la Reli mjini Tabora, ukiongozwa na Balozi Christopher Kasanga Tumbo.

Kipindi hicho, Nyerere alikuwa ameshaacha ualimu akiwa sasa kiongozi wa Tanganyika African National Union (TANU), akiendesha harakati za kutafuta uhuru. Lakini pia alivutiwa na harakati za Kawawa alivyohenyesha watawala kudai maslahi ya wafanyakazi.

### NYERERE AMSAKA

Kutokana na juhudi zake za kuendesha harakati za kudai maslahi ya wafanyakazi, Nyerere aliamua kumtafuta na mwaka huo wa 1955, walikutana katika jengo la makao makuu ya TANU.

Jengo hilo kwa sasa ndilo Ofisi Ndogo ya CCM Lumumba. Lengo la Nyerere kumwita lilikuwa kutaka washirikiane ili kuibana serikali ya kikoloni. Hakukuwa na ugumu wowote kukubaliana kwa kuwa Kawawa mwenyewe alikuwa akipenda harakati za Mwalimu Nyerere.

Tangu wakati huo, TANU na Chama cha Wafanyakazi vilikubaliana kwa ajili ya kuendesha harakati za siri kwa ajili ya kuwabana wakoloni waondoke nchini ili Watanganyika wajitawale.

Wakati wakiwa katika harakati hizo, Mwalimu Nyerere alimshawishi Kawawa ajiunge na TANU, mwanaharakati huyo alikubali ndipo ukawa mwanzo wa mageuzi. Alipewa nafasi ya kuwa Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria (LEGCO) kupitia TANU.

Kawawa aliaminika sana kwa Nyerere kwani muda mfupi baada ya uhuru, alimwachia uongozi wa nchi kwa muda, huku Nyerere mwenyewe akirudi kwenda kuimarisha TANU.

Leo, ikiwa ni kumbukumbu ya miaka 13 ya kifo cha mwanasiasa huyo, kuna mengi ya kumuenzi kutokana na mchango wake katika harakati za uhuru wa Tanganyika na mengi mengine aliyofanya kwa manufaa ya nchi.

### JASIRI ASIYESITA

Rashidi Mfaume Kawawa ambaye Nyerere alipenda kumwita kwa jina la Rashidi, alikuwa ni Waziri Mkuu wa Tanganyika mwaka 1962 wakati Nyerere alipokwenda mikoani kujenga chama na kufanya shughuli za kisiasa.

Kawawa alikuwa kiongozi shupavu aliyewahi kutokea, alikuwa kiongozi adhimu na mwenye moyo wa ajabu katika kuipigania nchi yake katika ufanyaji wa kazi mbalimbali za maendeleo.


Alikuwa mtu asiyeogopa kazi, hadharau kazi, hakuwa na makuu, makundi wala majungu, aliye chini yake akifanywa mkubwa kwake. Alifanya kazi kwa moyo wake wote na uwezo wake wote, bila manung'uniko au kinyongo.

Hakutaka mjadala kuhusu kilichoamuliwa, bali utekelezaji tu, hata pale Nyerere alipoonyesha kutoelewa au kutoafikiana na jambo fulani, alikuwa wa kwanza kutenda, kwa njia ya kurekebisha, ili liwe kama Nyerere alivyotaka.

Waliokuwapo mwanzoni mwa miaka ya 1970, watakuwa wanakumbuka jinsi alivyoamuru Umoja wa Vijana wa TANU kusimamia operesheni ya kuvaa nguo za heshima kwani wanawake waliovaa nguo fupi walikamatwa.

Ni Kawawa huyu huyu aliyesimamia mpango wa kugawa madaraka kwa Waafrika, aliyesimamia uanzishwaji wa vijiji vya ujamaa 'Operesheni Vijiji', ikiwa ni hatua mojawapo ya kutekeleza Azimio la Arusha. Vilevile, alisimamia kuanzishwa kwa maduka ya vijiji, ambayo yalilenga kutoa bidhaa kwa wananchi kwa ukaribu zaidi. Alikuwa haogopi kutekeleza uamuzi mgumu na kujikuta akiwa maarufu kwa jina la 'Simba wa Vita'.

Kwa ujumla alikuwa 'jembe' la Mwalimu Nyerere kutokana na utendaji wake na usimamizi wa majukumu yake kwa ujasiri wa hali ya juu, kwa ajili ya maendeleo ya nchi na watu wake.



Kawawa (kushoto) enzi za uhai wake akiwa na Rais wa kwanza wa Zambia, Dk. Kenneth Kaunda na Mwalimu Nyerere. **PICHA: MTANDAO.**

MAKALA

# 2022 ulishamiri watu kujichukulia sheria mkononi na kuwaua wenzao

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKA 2022 unafikia mwisho wake leo huku ukiwa umeacha makovu mengi. Hiyo ni kutokana na matukio mengi ya watu kujichukulia sheria mkononi na kuua ndugu zao, marafiki na hata wenza wao.

Hakuna wiki iliyoacha kusikika kuwapo kwa mauaji ya watu yakiwamo ya mume au mke kumuua mwezi wake sababu kubwa ikitajwa kuwa wivu wa mapenzi. Kila uchao makamanda wa polisi wa mikoa walikuwa wakipokezana kutoa taarifa za mauaji ya namna hiyo.

Mauaji ya kwanza yaliripotiwa kutokea mkoani Dar es Salaam baada ya Barke Rashid (30) kuawa Januari Mosi, huku tukio hilo likithibitishwa na Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam.

Tukio la pili lililothibitishwa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tabora, Richard Abwao, ni la kuuawa kwa mlinzi wa kiwanda kwa kupigwa shoka kichwani na mgongoni akiwa chumbani kwake, Januari 4.

Katika taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mtwara, ACP Marck Njera, ilielezea kutokea kwa mauaji ya mfanyabiashara Mussa Hamis, mkazi wa Kijiji cha Ruponda, Nachingwea Lindi, Januari 5.

Kama vile haitoshi, mwezi huo pia kuliripotiwa mauaji ya kikatili yaliyotokea Januari 10, 2022 eneo la Miches baada ya muuguzi wa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Rufina Komba, kukutwa ameuawa nyumbani kwake.



Dk Philip Mpango

Lakini pia Januari 17 kuliripotiwa mauaji ya mwanamke anayetajwa kwa jina la Teresia Maliya mkazi wa Ilboru wilayani Arumeru mkoani Arusha aliyedaiwa kubakwa na kunyongwa hadi kufa.

Matukio hayo yalikuwa kama yamefungulia mengine, yakiwamo ya watu sita wa familia moja kuuawa kwa kukatwa na mapanga sehemu mbalimbali za miili yao Julai 3, katika Kijiji cha Kiganza mkoani Kigoma.

**LHRC WATOA NENO**

Kutokana na mauaji hayo, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kiliweka wazi kuwa haki ya kuishi ndiyo iliyoongoza kukiukwa nchini katika mwaka huu wa 2022 ambao leo unafika mwisho.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, anasema katika maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu 2022, kwamba tathmini ya ufuatiliaji wa matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu inaonyesha kuwa matukio hayo yaliripotiwa na vyombo vya habari.

"Kwa mwaka huu tukitathmini kwa haraka haraka, haki za binadamu zilizovunjwa sana ni haki ya kuishi. Mauaji ya wenza yamekuwa mengi. Mauaji ya kujiua watu wenyewe yamekuwa mengi. Lakini pia, mauaji yanayotokana tu na imani za kishirikina na yamekuwa mengi," anasema Anna.




Anna Henga

Anataja mauaji hayo kuwa ni ya watu watano wa familia moja Dodoma yaliyotokea Januari 23 katika kijiji cha Zanka, wilayani Bahi, ambao walikutwa wameuawa ndani ya nyumba yao, huku miili ikiwa tayari imeharibika.

Anasema Mei 28, mtu aliyetambulika kwa jina la Said Oswayo, alidaiwa kumuua mkewe Swalha Salum (28) kwa kumpiga risasi kadhaa, nyumbani kwao eneo la Mbogamboga, Buswelu wilayani Ilemela, mkoani Mwanza.

Pia anasema Septemba 14, ziliibuka taarifa kutoka kitongoji cha Kibumbe, Kata ya Kiwira, Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya za mke, mume na watoto wawili kukutwa wamekufa ndani ya nyumba na miili yao ikiwa imeharibika.

"Novemba 23, 2022, Shani Yohana, mkazi wa Mbeya, alishikiliwa na polisi kwa madai ya kuwaua watoto wake wawili kwa kuwacharanga na mapanga hadi kufa, chanzo cha mauaji kikiwa hakijulikani," anasema.

**MPANGO AKERWA**

Kuendelea kwa mauaji hayo, kulimshutua Makamu wa Rais wa Tanzania Dk. Philip Mpango, na kuelezea kusikitishwa kwake na vitendo vya mauaji vilivyokuwa vikitokea na kuagiza Jeshi la Polisi kuingilia kati.

Kutokana na hali hiyo, aliimuagiza Mkuu wa Jeshi la Polisi kuingilia kati haraka na kukomesha mauaji ambayo yalikuwa yakishuhudiwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Akiwa katika kijiji ambacho mauji hayo yalitokea, Makamu wa Rais alitoa siku saba kwa IGP kuwakamata wote waliohusika na mauaji hayo. Alitaka mauaji hayo yafanyiwe kazi mara moja.

Makamu wa Rais alisema vyombo vya dola vifanye kazi, asibaki hata mtu mmoja, asakwe, wasakwe popote walipo, wachukuliwe hatua mara moja, huku akiitaka idara ya upelelezi ihakikishe wahusika wa mauaji wanabainika.

Waziri wa Mambo Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni naye aliwahi kukaririwa na vyombo vya habari, akisema katika kipindi cha kuanzia Januari Mosi hadi 15, matukio 22 ya mauaji yanayohusisha ndugu wa familia moja na wivu wa kimapenzi yameripotiwa, huku akiwataka viongozi wa dini kuisaidi serikali kuelimisha wananchi kuwa na hofu ya Mungu.



Muliro



# Darsh Industries inavyoipaisha pilipili mwendokasi kibiashara

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA ni miongoni mwa nchi chache za Afrika zenye uwezo wa kuzalisha na kujitosheleza kwa mazao yake ya chakula na biashara.

Tangu kupata Uhuru kilimo kimekuwa uti wa mgongo wa uchumi wa taifa, hii imesababisha kuikata minyororo ya wakoloni kwa haraka na kutoa fursa kwa watu kujiajiri na kuajiriwa.

Kilimo pia kimetoa fursa za ajira ya moja kwa moja kwa wataalam wenye ujuzi kama vile washauri, walimu au watafiti katika nyanja zao.

Pia kuna ajira za muda kama vibarua katika mashamba, usindikaji, uzalishaji, ufungashaji na idara za usafirishaji.

Takwimu zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 65 ya watu wanapata ajira katika sekta ya kilimo, iwe moja kwa moja au kwa njia nyingine, na uimara wa sekta ya kilimo unategemea uzalishaji wa mazao na upatikanaji wake.

Kilimo cha biashara, huchangia kuongezeka kwa mapato ya ndani kupitia michango ya kodi kwa serikali na kuwanufaisha wakulima kwa kutoa fursa za kuzalisha mapato.

Takwimu zinaonesha kuwa Sekta ya kilimo Tanzania inaingiza asilimia 30 ya mapato ya ndani, na kilimo cha biashara kupitia sekta ya usindikaji wa mazao ya kilimo kinakuza biashara kwa ujumla na kuwapatia wakulima soko mbadala la kuuza mazao yao moja kwa moja kwa wingi kwa viwanda vya ndani.

Zao la pilipili hoho limezidi kupata umaarufu kutokana na soko lake kuwa wazi na thabiti huku pilipili aina ya Mwendokasi zikifahamika zaidi.

Wakulima wanaolima zao hili la pilipili wameanza kuona mafanikio kutokana na kuongezeka kwa uhakika wa soko, ari ya ununuzi na usimamizi mzuri.

Wakulima waliohojiwa na timu ya waandishi wa habari kutoka Kituo cha Vyombo vya Habari dhidi ya Umaskini (MeCAP) wanasema zao la pilipili linakuwa kwa kasi na kuwa fursa kwao na limeondoa makali katika maisha yao.

MeCAP katika ziara yao walitaka kuchunguza jinsi wananchi wanavyonufaika na mazao ya biashara ili kupunguza umaskini, na jinsi kilimo cha pilipili Mwendokasi kinavyowasaidia wakulima.

Mikoa ya Arusha, Dodoma, Morogoro, na Iringa ilihusishwa na kote kulionekana pilipili Mwendokasi imeleta mageuzi katika biashara na kuwa chanzo kizuri cha kuwainua wakulima kiuchumi.

Baadhi ya wakulima wanasema kuna faida kubwa kutoka katika kilimo cha pilipili mwendokasi na kuchochea uchumi wao wa kila siku.

Uwepo wa kiwanda cha Darsh Industries Limited kama soko la kutegemewa umeibua shauku ya wakulima katika aina mpya ya zao la pilipili.

Darsh Industries Limited hununua na kusindika pilipili hizo kwa njia ya kisasa kupitia vifaa vyao vya hali ya juu vilivyoidhinishwa na taasisi ya kudhibiti ubora ya ISO.

Salum Mashaka mkazi wa Morogoro anayelima pilipili anaeleza kuwa imekuwa ni baraka kwake kuwa mmoja wa wakulima kwanza wanaonufaika na zao la pilipili mwendokasi tangu alipoanza kulima zao hilo kibiashara.

"Kwanza nitapata mbegu zenye ubora wa hali ya juu na kupata soko la uhakika kwa sababu kampuni ya Darsh Industries imekuwa ikinunua mazao yetu mara kwa mara, inatupa hamasa na usimamizi mzuri na hivyo kutuwezesha kuzalisha kwa ubora" anasema Mashaka.

Salome Mgeveke wa Iringa anasema pilipili za Mwendokasi zimemsaidia kupata uhakika wa fedha ili aweze kusomesha na kuwahudumia watoto wake wawili waliotelekezwa na baba yao.

"Inachukua kati ya miezi mitatu hadi mitano tangu kupanda hadi kuvuna kama mazao ikiwa yatatunzwa ipasavyo," anasema.

Mama huyo anasema hana wasiwasi tena ni wapi atapata ada ya mapacha wake kwa sababu pilipili ya Mwendokasi inamsaidia kukidhi mahitaji yake ya sasa.

Darsh Industries, ambayo pia hutengeneza bidhaa nyingine zinazotokana na usindikaji wa matunda na mboga mboga imekuwa ikifanya kazi na shirika la Uholanzi la Rijk Zwaan, kutoa ushauri na mbegu bora kwa wakulima ili kukuza kilimo cha pilipili nchini kote.

Darsh Industries imekuwa ikichakata Mwendokasi kwa njia ya kisasa na baadaye kuifunga kwa ufanisi, ili kuhakikisha mtumiaji anaweza kupata bidhaa zenye ubora wa hali ya juu.

Wachuuzi wa mitaani na wafanyabiashara wadogo wakiwemo wauza chipsi na mihogo wanaeleza kuwa pilipili Mwendokasi umeleta maendeleo makubwa ndani ya biashara zao.

Jamal Hoza, ambaye ni muuza chipsi kutoka Temeke jijini Dar es Salaam, anasema kuwa ubora wa mchuzi wa Mwendokasi umemsaidia kuongeza mauzo na kuongeza sifa yake kwa wateja wake.



TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kawa, mfuniko wa chakula na maneno ya mahaba, mipasho vilivyozimwa na ‘hotpot’

**Na Adam Fungamwango**



LEO tupo ukanda wa Pwani ambao kwenye miaka ya nyuma kulikuwa na kitu kinaitwa Kawa. Huu ni mfuniko maalum wa kufunikia chakula, uliokuwa ukitengenezwa kwa kusukwa na ukili.

Baada ya kusukwa uliwekwa rangi mbalimbali, nakshi tofauti kabla ya kuandikwa maneno ambayo mwenyewe aliyesuka au mnunuzi aliyapenda. Raha ya kawa ni lazima iwe na maneno kama ya kwenye kanga vile. Hebu kwanza tuangalie kawa ni nini?

Ni pambo la kifahari linalopendwa kutumiwa na wenyeji na wakazi wa maeneo ya ukanda wa Pwani. Wenyeji hao kutoka mikoa ya Pwani, Zanzibar, Dar es Salaam na Tanga ndio vinara wa mapambo hayo na walikuwa wakiona fahari kufunika zaidi msosi na kawa kuliko kitu kingine chochote.

Nikisema wakazi maeneo ya ukanda wa Pwani hata kama hawakuzaliwa huko, lakini kwa kukaa maeneo hayo kama nilivyoainisha, walikuwa wameshazoea na kujifunza utamaduni wa huko na wao wakajikuta wakiuendeleza. Na wenyeji ni wale ambao wamezaliwa ukanda huo ambao hao sasa ndiyo walikuwa vinara wa hayo.

Lakini raha ya kawa ni ujumbe wa maneno na maua yanayochorwa kwani hilo huwasilisha hisia zao kwa wapenzi wao au jamii inayowazunguka.

Mfano, mke anapomwandalia mume chakula au yeyote anayemwandalia mpenzi wake msosi, anafunika na kawa ambalo linakuwa na maandishi yenye ujumbe mbalimbali kama “Kula mwana ufurahie mapenzi”, “Ndoa ni heshima na uvumilivu”, “Nimekupata sitamani kukupoteza,” na ‘Kula zote zako mpenzi’, yote hayo yakiashiria mahaba na upana wake.

Ukiachana na kawa za kufunikia chakula, lakini yapo kwa ajili ya kupamba nyumba au unaweza kukuta sehemu za biashara zikining’inizwa ukutani na wapo wanaotumia kawa kusutana na kurushana roho kama ilivyokuwa kuvaliana khanga.

Unaweza kukuta mtu kaandika “Sili kwako maneno ya nini?”, “Wastara moyo wangu, uvumilivu dira yangu,” au ‘Mmenitafuta ya undani hamyapati,” ili mradi tu anayesoma anakutana na ujumbe uliokusudiwa.




Mbali na hayo, kuna simulizi kuwa katika mkoa wa Tanga hasa Tanga mjini, Muheza na Pangani, sanaa hiyo ya kutumia ujumbe kwenye kawa ilikuwa maarufu. Lakini ilikwenda mbali zaidi kutoka kwenye chakula na pambo la ukutani hadi kwenye mahaba.

Kihistoria, kuna dhana kwamba Tanga ndiko kwenye kitovu cha mahaba ndiyo maana wengi waliokwenda huko kufanya kazi kama vile: Bandarini na mashamba ya mkonge, walilowea huko kwa sababu ya kuzidiwa na penzi baada ya kuwaoa wanawake wa huko.

Inasemekana kwamba hata maji ya kuoga yalikuwa yakichemshwa huku yakiwa yamewekwa viungo kama: Iliki, ua waridi, mdalasini na karafuu kwa ajili ya kumwogesha mwanamume. Hayo yote ni chachandu katika mahaba.

Lakini maji hayo yalipokuwa yakifikishwa bafuni yakiwa kwenye ndoo, yalikuwa yakifunikwa kawa huku yakiwa na ujumbe mbalimbali kama vile “Moyo wangu umetua kwako”, “Sisikii la mwadhana, ni wewe tu” na mengine mengi

Mambo hayo hayakuishia hapo tu kwani simulizi zinabainisha kuwa hata katika chakula kuanzia kifungua kinywa, makawa yalikuwa yanatawala mezani yakiwa na ujumbe kama “Kula zote zako mpenzi”, “Tuleane hadi tuzeeke” na mengineyo mengi.

Twende sasa na jinsi kawa la chakula linavyofanya kazi. Baada ya msosi kupikwa na kuwekwa kwenye sinia au sahani, mwanamke atafunika chakula hicho na kawa lenye maneno murua ya mahaba ambayo ameyachagua kwa ajili ya mpenzi wake.

Atanyanyua chakula chake kutoka jikoni na kukipeleka sehemu husika. Na mara nyingi wanaume wa maeneo ya Pwani wao msosi wao wanalia kwenye mkeka.

Mgeni anapoingia kwenye nyumba hawezi kujua nini kimehifadhiwa ndani ya kawa au ni chakula gani na mara nyingi vyakula vya pwani huwa ni pilau, ugali, chapati, mikate, wali, samaki na vyakula vingine vinavyofanana navyo.

Chakula hicho kinaweza kuwekwa wakati mlaji yupo au hayupo. Anapokuja anakwenda kuoga na kuvaa msuli na kwenda sehemu ambayo mpenzi wake au mkewe ameweka chakula.

Kwanza kabisa kabla ya kula anakutana na maneno murua ya ujumbe wa mahaba ambao umewekwa hapo. Mwanamume anafarijika moyoni. Anakuwa anajua kabisa kuwa ujumbe ule unamhusu.




Anafunua kawa na kukutana na harufu nzuri ya chakula.

Mwanamume anakula chakula huku akifarijika kwa mwili na moyo. Kwanza ufundi wa msosi pamoja na maneno matamu ya kumtoa nyoka pangoni yaliyokuwa kwenye kawa.

Na kinamama wa wakati ule walikuwa wakibadilisha kawa kama nguo, kwani pamoja na kufunika chakula, lakini walikuwa wakihitaji zaidi maneno ya ujumbe ili kuwapelekea waume au wapenzi wao. Hata kama wamegombana na mwanamke kakasirika, unaweza ukaletewa chakula kimefunikwa na kawa iliyoandikwa “Kwetu sijaua mtu.” Sasa hapo inabidi uanze kufanya kazi ya ziada kuliokoa penzi, la sivyo lipo hatarini.

Mabadiliko ya teknolojia yana uzuri wake na changamoto zake. Kwa sasa vitu kama vyungu, mitungi, kata na mikeka kwa kiasi kikubwa vimeadimika sana si mijini tu, bali hata vijijini vimeanza kupungua. Mfuniko wa kawa nao umeingia kwenye mkumbo huo. Maeneo yote ya Pwani kwa sasa ni nadra sana kuuona.

Sasa hivi ni mwendo wa mabeseni, masufuria, mabakuli, vizuia joto maarufu kama ‘hotpot’ na vyombo vingine vinavyotengeneza kwa platiki au glasi ndiyo hutumika majumbani.

Watu wanapakua chakula na kukiweka kwenye vizuia joto. Mwanaume anakuja na kufungua chakula alichopika mkewe au mpenzi wake, hakuna ya ujumbe wala nini.

**Tuma meseji 0716 350534**

RIPOTI MAALUM

## KASI ONGEZEKO LA WATU

# Rais Samia, wataalamu wakuna vichwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

JUNI 1999 serikali ilianza kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, yenye dhima kuu ya kupunguza walau nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya waishi kwenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Hata hivyo, azma hiyo ya serikali iko shakani kutimizwa, ikiwa imebaki miaka mitatu kabla ya kufikiwa ukomo wa dira hiyo, kikwazo kikuu kikiwa ni kasi ya ongezeko la watu nchini.

Kwa mujibu wa Rais Samia Suluhu Hassan, matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, yanabainisha Tanzania ina watu milioni 61.74, wanawake wakiwa milioni 31.6 sawa na asilimia 51.

Mkuu wa Nchi anakiri idadi hiyo ni mzigo mkubwa kwa taifa, hivyo kutaka kuwapo mikakati madhubuti ya mipango ya maendeleo ya kutoa huduma huku akiwa na angalizo lingine kwamba makadirio yanaonesha ifikapo mwaka 2025, yaani miaka mitatu ijayo, Tanzania itakuwa na watu milioni 67.96.

Rais wa Awamu ya tatu, Hayati Benjamin Mkapa kupitia kitabu chake cha 'My Life My Purpose' (Kusudio la Maisha Yangu), anasisitiza ongezeko la watu ni tishio kwa maendeleo ya nchi na kushauri kuwe na mjadala wa kisera kulikabili.

"Ongezeko la watu katika nchi siyo kipimo cha maendeleo, bali ni kikwazo kwa maendeleo. Shida kubwa ya nchi nyingi za Kiafrika hatuna mjadala madhubuti kuhusu sera ya idadi ya watu katika nchi zetu," Mkapa analalamika kwenye kitabu chake hicho.


Anagusia ubashiri wa kisayansi wa mwelekeo wa sensa zijazo kwamba kufikia mwaka 2025, ambao ndiyo ukomo wa Dira ya Maendeleo ya Taifa (1999-2025), nchi itakuwa na wakazi milioni 67 kama ilivyobainishwa na Rais Samia. Tanzania ina eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 947,300.

Katika kitabu chake hicho, Mkapa anabainisha kuwa wakati wa uhuru mwaka 1961, kulikadiriwa kuwapo Watanganyika milioni 10.4 na idadi iliongezeka hadi Watanzania milioni 27.4 alipoanza kukalia kiti cha urais mwaka 1995 na iliongezeka hadi watu milioni 36.1 alipoondoka madarakani mwaka 2005.

Vilevile, Ripoti ya Juni 21, 2017 ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA) ilibainisha Tanzania imo kwenye orodha ya nchi tisa zinazochangia kasi ya ongezeko la watu duniani, ikitangazwa kuwa ya nne barani Afrika.

HALI ILIVYO

Katika ufafanuzi wake wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Rais Samia anasema Tanzania ina watu milioni 61.74. Kati yao, milioni 59.85 wapo Tanzania Bara na milioni 1.88 wapo Tanzania Zanzibar.




Idadi hiyo inajumuisha wanawake sawa na asilimia 51 na wanaume milioni 30.5 sawa na asilimia 49 ya watu wote.

Takwimu hizo zinatoa fasili ya kuwapo ongezeko la watu milioni 16.81 katika kipindi cha miaka 10 iliyopita kwani Tanzania ilikuwa na watu milioni 44.92 mwaka 2012 sawa na ongezeko la asilimia 3.2.

Takwimu hizo pia zina maana kwamba kwa Tanzania Bara idadi ya watu imeongezeka kutoka milioni 43.62 mwaka 2012 hadi watu milioni 59.85 mwaka huu na kwa Zanzibar idadi ya watu imeongezeka kutoka milioni 1.3 mwaka 2012 hadi milioni 1.8 mwaka huu, sawa na ongezeko la asilimia 3.7.

Kwa mujibu wa Rais Samia, Tanzania ina jumla ya majengo milioni 14.34. Kati yake, Tanzania Bara ni milioni 13.9 na Tanzania Zanzibar ni 440,421 huku nchi ikiwa na vituo vya afya 10,067 (zahanati 7,889, vituo vya afya 1,490 na hospitali 688). Tanzania pia ina shule 25,626. Kati yake, za msingi ni 19,769 na sekondari 5,857.

**JICHO KITAALUMA**

Mchambuzi wa masuala mbalimbali, Dk. Nasibu Mramba anasema matokeo ya sensa hiyo yatumike vizuri kwa kuwa nchi sasa ina takwimu sahihi za idadi ya watu zitakazosaidia kwenye mipango ya maendeleo badala ya kuenenda kwa makisio.

"Katika kuangalia ukuaji wa nchi upo kwa kiasi gani au kipato cha mtu ni kiasi gani, tunapoangalia uchumi kwa ujumla tunagawanya na idadi ya watu. Kama unakosea idadi ya watu, unapata jibu ambalo siyo sahihi. Kwa sasa ukisema kipato cha mtu ni kiasi gani kwa mwaka unakuwa upo sahihi.

"Idadi yetu inaongezeka kwa asilimia 3.2 kwa miaka 10, tunatakiwa kuhakikisha kwenye kila miaka 10 vitu vinaongezeka kwa asilimia hiyo. Kwa mfano, kama ni barabara ziongezeke ka asilimia angalau tatu, shule, vituo vya afya, yaani kila kitu kiangalie watu watakavyokuwa wanaongezeka," anasema.

"Siyo Tanzania tu, ukilinganisha dunia na Afrika idadi ya watu inaongezeka sana Afrika. Sasa ongezeko la watu lina faida na hasara. Kwa upande wa faida unapata nguvukazi na uhakika wa soko la bidhaa, na hasara ni kwamba inatakiwa ukuaji huo uende sambamba na ukuaji wa rasilimali, lakini kuna rasilimali huwa hazikui ikiwamo ardhi, hivyo tuzae kwa mpango," anashauri.

Ofisa Mipango Miji wa Jiji la Dodoma, Azor William anasema ongezeko la watu linatengeneza mahitaji, akifafanua: "Unatakwiwe na huduma za kijamii - shule, afya, miundombinu, makazi, huduma za maji, umeme na vitu vyote vinahusiana na ardhi. Kwa hiyo, wakiongezeka wanahitaji shule kadhaa ziongezeke, vituo vya afya viongezeke."

William anasema ardhi huwa haikui wala kuongezeka na madhara ya ongezeko hilo yapo kwenye mazingira, uchumi na jamii.

"Kwenye mazingira ongezeko la watu, kama mipango miji haijafanyika, inaweza kusababisha kuibuka kwa makazi holela, migogoro ya ardhi, watu kuvamia maeneo ya watu, watu kutokuwa na sehemu za kutupa taka," anasema.

Kuhusu faida, ofisa huyo anasema ongezeko hilo linatengeneza fursa nyingi za uhitaji wa makazi yaliyopangwa vizuri, fursa za uwekezaji wa shule, masoko makubwa na biashara kukua.

Profesa aliyebobea katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Pius Yanda anasema ongezeko hilo la watu nchini litasababisha uhitaji mkubwa wa huduma za kijamii ikiwamo maji, ardhi na chakula ambazo nazo upatikanaji wake tayari umeshaanza kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

"Tunaona hizo rasilimali nazo zina changamoto. Kwa mfano, huwezi kuzalisha chakula kama mvua haitabiriki na hakuna ardhi ya kutosha. Kwa sasa tunapitia changamoto ya ukame na uharibifu wa mazingira ikiwamo mmonyoko wa udongo," anafafanua.

Prof. Yanda anasema kutokana na ongezeko hilo la watu, ni wazi sehemu kubwa ya ardhi itatumika kwa ajili ya kilimo, ikizingatiwa kuwa asili ya kilimo nchini imejikita zaidi kwenye ardhi kwa kuwa jamii haina uwezo wa kulima kisasa.

Anatoa angalizo kuwa ongezeko hilo la watu litachangia uharibifu wa mazingira kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu ikiwamo kukata miti kwa ajili ya nishati kama kuni na mkaa pamoja na kujenga nyumba kwa ajili ya makazi.

Prof. Yanda pia anasema nchi itegemee idadi kubwa ya watu kuhama kutoka vijijini kwenda mijini, wakiamini watapata kazi na maisha yao kuwa mazuri, hali itayaoongeza ugumu wa upatikanaji wa huduma za kijamii.

"Mfano mzuri ni sasa ambapo upatikanaji wa maji umeshaanza kuwa wa shida, kwa sababu yaliyopo hayatoshelezi kukidhi mahitaji la wakazi wote, hivyo kusababisha kuwapo na mgawo," anafafanua.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, Dk. Fabian Massaga anasema mfumo wa huduma za afya ulivyo nchini kuanzia vituo vya kata, wilaya hadi hospitali za rufani zimetengenezwa kulingana na idadi ya watu na wataalamu watakaokuwapo katika vituo husika.

Anasema kuongezeka kwa idadi ya watu kuna maana kwamba utoaji huduma unatakiwa kuongezwa rasilimali watu, vitendea kazi pamoja na miundombinu ili kutoa huduma iliyo bora kwa watu wote.

Daktari katika Kituo cha Afya Kisesa mkoani Mwanza, Daudi Zimulinda anasema ongezeko hilo la watu linachangia uhitaji wa huduma za afya kuongezeka, hivyo bajeti ya serikali kwenye huduma za afya inabidi iongezwe ili kukidhi mahitaji ya wananchi.

Anashauri elimu ya afya itolewe kwa wingi ili kupunguza magonjwa ya mlipuko na mengineyo ili kuepuesha vituo visizidiwe na idadi ya wagonjwa.

"Lishe bora izingatiwe, matumizi ya pombe na matendo hatarishi kwa afya yaepukwe, itasaidia kuepukana na magonjwa ya mara kwa mara kwa watoto na watu wazima.

"Kwa ongezeko ilo la watu idadi ya wanaokwenda hospital kwa mwezi itaongezeka tofauti na miaka ya nyuma, hivyo ni lazima watumishi waongezwe pamoja na vituo vya afya, kila kitu lazima kiongezwe.

"Kutokana na ongezeko hili la watu, ni wazi idadi ya wanawake wanaopata ujauzito itaongezeka, hivyo huduma za mama na mtoto ziboreshwe ili kuondokana na vifo vya uzazi na kuwa na uzazi salama," anashauri daktari huyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VYETI VIMEPOTEA



**NDG.YOHANA SAMWELI MPAYO.** Anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo: Cheti cha kidato cha Nne (IV), chenye **Index na.S0457-0114** cha mwaka 2006 na Cheti cha kidato cha Sita (VI),chenye **Index na.S0457-0566** cha mwaka 2011,vyote vilitolewa na Baraza la mitihani Taifa kupitia shule ya sekondari Igawilo-Mbeya.

Kwa yeyote atakayeviona anaombwa aripoti kwenye kituo chochote cha polisi kilicho karibu.

RIPOTI YA **POLISI/MBE/MBE/RB/279278/2022**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PRISCA HENJEWELE MOLLEL** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T176CZS** aina ya Nissan DUALIS. Chassis No. **NJ10006343,** Engine No. **MR20269718A.** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya polisi

**DOD/DOD/RB/496670/2022**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO..... 2022**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE BEATUS ALKADO MALEMA**
**Of Miyuji within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY IVONA AGUSTINO KALENZI**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 07 Day of 12, 2022

Date at Dodoma this 08 day of 11, 2022

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA AT BUKOBA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 05/2022**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE CYRIACUS FRANCIS BAYOBA AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION OF ESTATE BY JOSEPHINA PASCHAL**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they thinks fit before the grant of the letter of administration is made to the above - named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15th day of February 2023.

Dated at Bukoba this 02nd day of December, 2022.

REGISTRAR

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.157/2022**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ANDREA KISOLE**
**Of Area A within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY BALEMA ANDREA KISOLE AND NEEMA ANDREA KISOLE**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 6th Day of January, 2023

Date at Dodoma this 5th day of August, 2022

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTELEWA NA CHETI

**ENVIRONMENT IN LIFE AND PEACE OF MIND** inatangaza kupotelewa na cheti cha usajili chenye namba za usajili **No.12600** kilichotolewa na **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI** mwaka 2004, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi taarifa

**DAR/MAG/RB/488659/2022**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kiburi cha kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi waliyouziwa na mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haitoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kuwanyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja ya wasichana warembo kijijini hapo ni miongoni mwa waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# Mtake Msitake-12

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Ukweli ni kwamba, Usonzo alionekana kumuonea huruma Adel kwa maneno, lakini machoni hakuonekana hivyo. Uso wake ulionekana kuwa wa kejeli na dharau. Na alifanya hivyo makusudi akijua Adel hawezi kujua kwa sababu haoni.

"Ni kweli bosi wangu kwa sababu vitabu vya Mungu vinasema samehe saba mara sabini. Mimi sina kinyongo, Mary ni rafiki yangu nilifahamiana naye siku chache tu tangu naingia katika kijiji hiki, lakini kilichotokea naona kama shetani tu alipita kati yetu." Akajibu bila kujua kuwa alikuwa anang'ong'wa.

"Sasa kijana ni hivi, mimi ndiyo niliyetoa pesa kwa ajili ya familia yako hapa kijijini, bibi yako na ndugu zako wengine. Pia leo nitakupa kiasi cha shilingi milioni moja kama pole. Mwezi mmoja na nusu hivi ujao tumepanga mimi na Mary kukupeleka Muhimbili kwa ajili ya matibabu zaidi. Kwa mujibu wa madaktari ni kwamba unaweza kuona tena kama utapelekwa kwenye hospitali zenye vipimo vya kisasa. Kwa hiyo, utaondoka hapa ukiambatana na mimi pamoja na Mary, sawa?"

"Nitashukuru sana bosi wangu, na ndiyo maana naendelea kuamini kuwa Mary alipitiwa, na kitu ambacho si cha kawaida kufanya tukio hili, haikuwa dhamira yake ya dhati. Mimi binafsi kabla ya kufika hapa nimeongea na Mary na nimekubaliana nalo hilo. Nitakwenda kwenye matibabu na nina amini nitaweza kuona tena."

Kwa sababu mhusika tayari alikuwa ameshakubaliana na kila kitu, hakukuwa na cha ziada na kwa sababu ameshakaa muda mrefu, Mary na Adel wakamuaga Usonzo, mfadhili wa safari na matibabu.

Walitoka mlangoni, lakini ni kama kuna kitu alisahau, akamwambia Adel asimame. Akarejea ndani na kuteta.

"Haya sasa kila kitu kimekamilika, kazi kwako."

"Yaani mimi nilivyofurahi Mary sikwambii kitu. Nataka nikuchukue moja kwa moja uwe mke wangu."

"Mimi huyo?"

"Nani mwingine?"

"Haya baba uamuzi ni wako, kuchemsha, kukaanga au kula chukuchuku."

********************************

"Hivi unajua zamani nilidhani mtu akiwa anakaa Dar es Salaam anakuwa na akili kushinda watu wa mikoa mingine na vijijini."

"Kwa nini Maliza?"




**"Sikiliza Mona. Mimi nisingeweza, kwani yule kwao hana. Hapa kijijini si alikuja kwa bibi yake, bibi Anna Msafiri. Yaani kahama kabisa na kwao. Anakaa kwa huyo huyo adui yake. Mtu hakupendi, keshakufanya umekuwa kipofu, sasa nini si angerudi tu Dar es Salaam."**

"Huyo ndugu yenu huyo, wanamwita nani vile, Adel."

"Kafanyeje?"

"Mwanamke umemuokoa kwenye ajali ya bodaboda, halafu fadhila yake kakumwagia tindikali, umeshakuwa kipofu, bado tu unakubali kukaa kwao, halafu anakusanifu anakutembeza sehemu yote kwa kukushika mkono, hii ni fadheha hii!"

"Maliza huwezi kujua nini kaambiwa, hayo ni masuala yao binafsi."

"Sikiliza Mona. Mimi nisingeweza, kwani yule kwao hana. Hapa kijijini si alikuja kwa bibi yake, bibi Anna Msafiri. Yaani kahama kabisa na kwao. Anakaa kwa huyo huyo adui yake. Mtu hakupendi, keshakufanya umekuwa kipofu, sasa nini si angerudi tu Dar es Salaam."

Mazungumzo hayo yalikuwa baina ya Maliza na mpenzi wake Mona baada ya kuwashuhudia Mary na Adel wakipita mtaani kwao.

Mary alikuwa amemshika mkono akimuongoza Adel aliyekuwa amevaa miwani myeusi, lakini haoni. Ameshakuwa kipofu.

Kitendo cha Adel kuendelea kukaa kwa Mary na hata kuendelea na urafiki na mchumba wake Enock bado kiliendelea kuwashangaza wengi.

Baadhi walikwenda hadi kwa bibi yake Adel ambaye bado alikuwa akiendelea kuumwa, wakaongeza na ndugu zake kuwa wakamuondoe ndugu yao kwenye mikono ya Mary na mchumba wake Enock, vinginevyo sasa hali inavyoendelea wanaweza kumuwekea sumu wakamuua kabisa.

Wakazi wa kijiji hicho wakashangazwa pia na kasi ndogo au iliyokufa kabisa ya ufuatiliaji wa tukio lile. Walitegemea mpaka kufikia wakati ule, tayari Mary angekuwa ameshatiwa nguvuni.

"Hivi unajua Mary ameamua kumng'ang'ania Adel kwa ajili ya kujilinda tu asikamatwe na si vinginevyo, ila anayeumia ni yule kijana maskini. Angekuwa ndugu yangu asingekuwa pale." Maliza aliendelea kumpasha mpenzi wake. Halafu akauliza.

"Hivi yule kijana ana muda gani kwenye kijiji hiki? Maana nyinyi wanawake ndiyo mnaojua mengi sana."

"Mwanaume wewe naye kwa umbea. Yaani umekaa kazi kumzungumzia mwenzako tu, subiri na wewe yakukute.

Yule ana miezi sita hapa, alikuja kwa ajili ya kumchukua bibi yake ili ampeleke Dar kwa matitabu, lakini alimkuta mahututi, wakampeleka kwanza kwenye zahanati ili apate ahueni. Na kweli bibi akapata ahueni kiasi kwamba ikabidi sasa waahirishe kwanza. Lakini unajua tena ujana, kakutana na mrembo Mary, yakatokea ya kutokea, kamuokoa kwenye ajali, akadhani atapata fadhila ya kupewa anachohitaji kaishia kuwa kipofu." Mona alisema huku akiwa anamshikashika mpenzi wake kidevu.

Miezi mitatu si mingi. Wiki mbili kabla ya kutimia miezi mitatu, Adel alikuwa akipita sehemu mbalimbali akiaga kuwa ataondoka kijijini hapo wiki mbili zijazo.

Habari hizi ziliwahuzunisha wanaompenda na kuwafurahisha wanafiki. "Kaja na macho anaondoka kipofu. " Mmoja aliongea pembeni na mwenzake.

Hakuwaambia wanakijiji kama anaondoka hapo kwenda kutibiwa kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, badala yake akasema tu anaondoka.

Kilikuwa ni kipindi kizuri mno kwa Usonzo kwani alijua ndiyo wakati wa kumuweka kwenye himaya mtoto mzuri na mrembo, Mary.

Msichana wa ndoto yake. Tajiri kama yeye ndiye anayepaswa kuwa na msichana kama huyo na si kinyago mwingine yoyote.

"Mpenzi nataka tufanye sherehe kubwa kijiji hapa."

"Ya nini mpenzi?"

"Yaani si tunaondoka hapa, umesahau? Au umeahirisha mipango? Sisi tuseme ya kumuaga Adel, lakini moyoni mwetu ni ya kuwaaga wanakijiji na kuondoka."

"Nasema kila siku wewe ni mwanaume mwenye akili sana, na kweli, mimi nitagharamia kila kitu. Tufanye sherehe kubwa ya kumuaga Adel ndugu yetu anaondoka, halafu tunaondoka naye kumpeleka kwenye Hospitali ya Muhimbili kisha kumtelekeza kama mpango wetu tulivyopanga."

"Na baada ya hapo na sisi tunatokomea. Tunakwenda kuishi Arusha si ndiyo mpenzi?"

"Haswa na mimi huku tena nitakuwa natuma tu mwakilishi, sina mpango wa kurudi tena huku, mambo yote yatakuwa yanasimamiwa na watu wangu."

"Urudi kufanya nini, Henock atakuacha kweli?" Alipomaliza kusema hivyo, wakaangua kicheko.

"Yaani imebaki wiki mbili naona kama mwaka mtoto we, nilikuwa na hamu na wewe." Usonzo akafunguka.

"Anza kufanya mazoezi kabisa, wiki mbili tu zimebaki na mimi kumaliza dozi yake ya dawa ya tumbo niliyokwambia, kila kitu kimekwenda kama kilivyopangwa."

Siku mbili baadaye Mary na Adel walikwenda tena ofisini kwa Usonzo kumshukuru kwa kutoa kitita cha pesa ambacho kitafanikisha matibabu yake na nauli pia.

Wakati akiongea maneno matamu ya kumuaga mfadhili, Mary na Usonzo walitazamana na kukonyezana kwani wanajua hakukuwa na mpango wowote ule, bali wanachotaka kufanya ni kwenda kumtelekeza hospitali ili wapate nafasi ya kwenda kula raha. Kwenda Arusha kula nchi, kula kuku hadi bata waone wivu, kula kuku na mifupa yake na kula kuku kwa mrija.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# AZAM YAAHIDI KUMALIZA HASIRA KWA MBEYA CITY

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kupata kichapo cha mabao 3-2 kutoka kwa Yanga, Azam FC imepania kumaliza hasira zake kwa kuifunga Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Aggrey Morris, alisema kikosi chao kimejipanga vyema kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo na kurejea kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Morris alisema wanawafahamu vyema wapinzani wao na wamejiandaa kukutana na changamoto mbalimbali katika mechi hiyo. Beki huyo wa zamani wa timu hiyo alisema malengo ya Azam FC ni kupata pointi tatu na watacheza kwa tahadhari kuhakikisha wanafikia malengo.

Alisema wachezaji wote wako vizuri na wamerekebisha makosa yaliyojitokeza katika mechi iliyopita ili kuvuna matokeo bora watakapowavaa ya Mbeya City.

"Mchezo uliopita tulifanya makosa ambayo yalituadhibu, tayari tumeyafanyia kazi, ninaamini hayatajirudia katika mechi ya kesho (leo)," alisema kocha huyo.

Aliongeza katika mechi hiyo watawakosa wachezaji wao watatu ambao wamepata matatizo ya kifamilia.

Naye Kocha Msaidizi wa Mbeya City, Anthony Mwamlima, alisema amekiandaa kikosi chake vizuri kisaikolojia na kimwili ili kuhakikisha hawapotezi pointi.

"Nimewaandaa vizuri wachezaji wangu kisaikolojia, kila mchezaji atahakikisha atatimiza majukumu yake, tutacheza kwa tahadhari ili tusiupoteze mchezo huo muhimu," alisema Mwamlima.

Aliongeza wanawaheshimu wapinzani wao kutokana na aina ya kikosi walichonacho na alikiri mchezo huo unatarajiwa kuwa wenye ushindani.

## Mashabiki 50 waula na 10bet

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wa soka 50 wamepata zawadi mbalimbali kutoka katika Kampuni ya michezo ya kubahatisha ya 10bet baada ya kuibuka washindi wa promosheni ya Kombe la Dunia iliyojulikana kwa jina la World Cup Bonanza Promotion, imeelezwa.

Michuano ya Kombe la Dunia ilifanyika nchini Qatar na Argentina chini ya nahodha wake, Lionel Messi ilitwaa ubingwa.

Meneja Masoko wa Kampuni ya 10bet Tanzania, George Abdulrahman, alisema kati ya washindi hao 50, washindi 10 walizawadiwa simu janja huku wengine 20 walizawadiwa jezi za timu za mataifa mbalimbali yaliyoshiriki michuano hiyo na washindi 30 walizawadiwa fedha taslimu.

Abdulrahman alisema washindi hao wamepata zawadi baada ya kufanikiwa kupata pointi nyingi kati ya maelfu ya mashabiki wa soka waliokuwa wakibashiri matokeo mbalimbali wakati wa michuano hiyo ikiendelea na tayari washindi hao wamekabidhiwa stahiki zao.

"Tunajisikia fahari kubwa kuwazawadia mashabiki wa soka walioshiriki kwa kubashiri kupitia michezo yetu mbalimbali," alisema Abdulrahman.

Bosi huyo aliwaomba mashabiki wa soka wenye umri kuanzia miaka 18 kushiriki kubashiri na kampuni yao ili kushinda zawadi mbalimbali pamoja na fedha taslimu.

"Tunawaomba mashabiki kuendelea kubashiri na kampuni yetu ambapo mbali ya fedha, wataweza kushindia zawadi mbalimbali.




Adali Hamidu, mmoja wa washindi wa promosheni ya Kombe la Dunia iliyoandaliwa na Kampuni ya Kubashiri ya 10bet Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mbeya Kwanza FC yaendeleza makali

**Na Adam Fungamwango**

MBEYA Kwanza FC imeweka rekodi ya kushinda mechi saba mfululizo katika Ligi ya Championship inayoendelea kwenye viwanja mbalimbali hapa nchini ili kusaka timu zitakazocheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Ushindi wa bao 1-0 ilioupata dhidi ya Biashara United katika mechi ya juzi umeifanya timu hiyo kufikisha ushindi wa saba mfululizo, ikiwa ni timu pekee iliyofanya hivyo kwenye ligi hiyo msimu huu.

Mara ya mwisho timu hiyo ilipoteza mechi Oktoba 29, mwaka huu ilipofungwa mabao 2-0 dhidi ya Kitayosce, lakini baada ya hapo ilicharuka na kuanza kutoa vipigo kwa kila timu waliyokutana nayo.

Hata hivyo, pamoja na kushinda mechi zote hizo, Mbeya Kwanza iliyocheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/22 na msimu huo huo kushuka, inashika nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 27 baada ya kushuka dimbani michezo 14.

Mpaka sasa ligi hiyo inaongozwa na Maafande wa JKT Tanzania wenye pointi 34, Kitayosce ikifuatia kwa kujikusanyia pointi 32 na Pamba ikiwa katika nafasi ya tatu ikimiliki pointi 28.

## Kitila mgeni rasmi Kombe la Ubungo

**Na Shufaa Lyimo**

MBUNGE wa Jimbo la Ubungo, Kitila Mkumbo, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la vijana la Wilaya ya Ubungo ( UFa CUP) itakayofanyika kesho kwenye Uwanja wa Kinesi, Dar es Salaam.

Mabomba FC watakutana na Makuburi katika mechi hiyo ya fainali ambayo mshindi atazawadiwa Sh. 300,000 pamoja na jezi na mipira miwili.

Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Wilaya ya Ubungo (UFA), Frank Mchaki, alisema awali fainali hiyo ilipangwa ifanyike tangu Septemba, mwaka huu lakini iliahirishwa kutokana na msiba wa aliyekuwa mwenyekiti wao, Benjamin Mwakasonda.

Mchaki alisema maandalizi ya fainali hiyo yako katika hatua za mwisho na mshindi wa pili atapata zawadi ya Sh. 100,000.

Aliwataka vijana kutoka sehemu mbalimbali wajitokeze kushuhukia mechi hiyo ambayo inatarajiwa kuwa na ushindani.

## ZISIKUPITE

### LOCATELLI ATAJWA MADRID

REAL Madrid imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Italia, Manuel Locatelli, mwenye umri wa miaka 24, ambaye yuko kwa mkopo Juventus kutoka Sassuolo, ikiwa watamkosa, Jude Bellingham au Enzo Fernandez. ***(AS)***

### FOFANA KUTUA CHELSEA

CHELSEA imefikia makubaliano ya mkataba wa euro milioni 12 na Molde ili kumsajii mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, David Datro Fofana, mwenye umri wa miaka 20. ***(Fabrizio Romano)***

### MENDY AGOMEA MKATABA

GOLIKIPA wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Senegal, Edouard Mendy, mwenye umri wa miaka 30, amepuuza mbali mkataba mpya wa miaka sita pale Stamford Bridge kwa sababu anaamini klabu hiyo haimwonyeshi "heshima" ya kutosha linapokuja suala la mshahara. ***(Sun)***

### ARSENAL: TUNAMTAKA MUDRYK

OFISA Mkuu Mtendaji Mkuu wa Shakhtar Donetsk, Carlo Nicolini, amethibitisha Arsenal imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ukraine, Mykhailo Mudryk, mwenye miaka 21. ***(Calciomercato)***

### RABIOT ATAJWA ARSENAL

ARSENAL itajaribu kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Adrien Rabiot, mwenye umri wa miaka 27 ambaye mkataba wake utamalizika Juventus msimu wa joto. ***(Repubblica, via Mail)***

### SOARES AGOMBEWA ULAYA

KLABU ya Arsenal bado haijaamua iwapo itamruhusu mlinzi wa Ureno, Cedric Soares kuondoka Januari, huku Fulham ikiongoza mbio za kumsaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ambaye pia anawavutia Bayer Leverkusen na Villarreal. ***(Evening Standard)***

### UNITED YAMTAKA EMILIANO

KLABU ya Manchester United imeonyesha nia ya kumsajili mlinda mlango wa Aston Villa, Emiliano Martinez, mwenye miaka 30, ambaye alichangia kuisaidia Argentina kushinda taji la Kombe la Dunia. ***(Football Insider)***

### SERIKALI YAMTAKA RONALDO

OFA ya Al-Nassr ya mkataba wa pauni milioni 160 kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo, mwenye umri miaka 37, inaungwa mkono na serikali ya Saudi Arabia. ***(Ben Jacobs via Express)***

### JUDE AITAKA MADRID

KIUNGO wa kati wa England, Jude Bellingham anapendelea kujiunga na Real Madrid kutoka Borussia Dortmund, licha ya Liverpool, Manchester City na Manchester United kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19.***(AS)***

### THAMANI YA ENZO YATAJWA

BENFICA imekataa ofa ya euro milioni 100 kutoka kwa klabu ambayo haijatajwa jina kwa ajili ya kiungo wa kati wa Argentina, Enzo Fernandez, ambaye amekuwa akihusishwa pia na Liverpool na Real Madrid. Imesema haitamuuza nyota huyo mwenye umri wa miaka 21 kwa dau la chini ya euro milioni 120. ***(Record)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BRAZIL YATANGAZA SIKU 3 MAOMBOLEZO YA PELE

Familia pekee ndio itahudhuria mazishi nyota huyo atakayezikwa katika kaburi la wima...

**SAO PAULO, Brazil**

BRAZIL imetangaza siku tatu za maombelezo baada ya kifo cha gwiji wa soka wa nchini humo na duniani, Pele, ambaye bila shaka ndiye mchezaji bora zaidi kuwahi kutokea, amefariki akiwa na umri wa miaka 82.

Pele anasifiwa kwa kufunga mabao 1,281 katika rekodi ya dunia katika mechi 1,363 katika kipindi cha miaka 21 ya maisha yake, yakiwamo magoli 77 katika mechi 92 za nchi yake.

Pele ndiye mchezaji pekee aliyeshinda Kombe la Dunia mara tatu, akinyakua taji hilo mwaka 1958, 1962 na 1970 na alitangazwa mchezaji bora wa karne na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA) hapo mwaka 2000.

Nyota huyo alikuwa akisumbuliwa na matatizo ya figo na kibofu katika miaka ya hivi karibuni.

Uwanja ambao nguli Pele alicheza baadhi ya mechi bora zaidi za maisha yake pia utaruhusu watu kutoa salamu zao za mwisho siku ya Jumatatu na Jumanne.

Santos, klabu ambayo Pelé alicheza huko Brazil, ilisema katika taarifa umma utaweza kutoa heshima zao za mwisho kwenye Uwanja wa Vila Belmiro, nje ya Sao Paulo.

Pelé, ambaye jina lake kamili ni Edson Arantes do Nascimento, alifariki Alhamisi baada ya kuugua saratani kwa muda mrefu.

Santos ilisema jeneza litakalombeba bingwa huyo mara tatu wa Kombe la Dunia litaondoka katika hospitali ya Albert Einstein mjini Sao Paulo mapema Jumatatu asubuhi na litawekwa katikati ya uwanja.

Mazishi yatafanyika kwenye makumbusho ya Necrópole Ecumênica, kaburi la wima huko Santos.

Familia pekee ndiyo itahudhuria na Pelé ana nyumba huko Santos, ambako aliishi zaidi wakati wa uhai wake.

Pele alifanyiwa upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye utumbo wake mnamo Septemba, mwaka jana katika Hospitali ya Albert Einstein, Sao Paulo, baada ya uvimbe huo kugunduliwa katika vipimo vya kawaida.

Alirejeshwa hospitalini mwishoni mwa Novemba mwaka huu.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,062,0

MECHI KALI
WOLVERHAMPTON
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 3.79
X | 3.35
2 | 1.93

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ANCELOTTI AMKATAA MESSI



**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti amekataa nahodha wa timu ya taifa ya Argentina na PSG ya Ufaransa, Lionel Messi ni mchezaji bora wa muda wote.

Ushindi wa Kombe la Dunia wiki kadhaa zilizopita ulimpa Messi taji moja ambalo ndio taji pekee ambalo alibakisha katika maisha yake ya mpira.

Mshindi huyo mara saba wa tuzo ya Ballon Dor, baada ya kubeba taji hilo watu wengi walisema inawezekana Messi ndio mchezaji bora wa muda wote kutokea katika mpira wa miguu.

Ancelotti alipoulizwa kama Messi ndio mchezaji bora wa muda wote yeye alijibu kwa kusema ni kazi ngumu sana kukiri hilo.

Huku akisema awe ameshinda Kombe la Dunia au la, lakini kazi yake bado inaendelea.

"Kwenye kila kizazi kunatokea wachezaji wenye nguvu, lakini kusema Messi ndio bora katika historia hiyo haitotokea kwenye kinywa changu," alisema kocha huyo ambaye anatajwa sana kurithi mikoba ya Tite kwenye Timu ya Taifa ya Brazil.

Ancelotti amesema amewashuhudia wachezaji wengi wenye ubora amesema amemwona, Diego Maradona, Johan Cruyff na sasa anamfundisha mshindi wa tuzo ya Ballon Dor, Karim Benzema hivyo yeye hajui nani ni mchezaji bora kuwahi kutokea.

# Jorginho apewa mkataba mpya

**LONDON, England**

JORGINHO amepewa mkataba mpya na Chelsea huku kukiwa na uvumi anatakiwa na klabu kadhaa, kwa mujibu wa wakala wa kiungo huyo.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Italia, ambaye amekuwa katika kikosi cha kwanza cha Chelsea kwa misimu mitano iliyopita, anatarajiwa kuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu.

Barcelona na Juventus wanaripotiwa kuonyesha nia ya kufanya mazungumzo na Jorginho hapo Januari, huku wapinzani wa Chelsea katika Ligi Kuu England, Newcastle United pia wakihusishwa na mchezaji huyo wa zamani wa Napoli.

Hata hivyo, wakala wa mchezaji huyo, Joao Santos, amefichua nyota huyo mwenye umri wa miaka 31 atazungumza kwanza na Chelsea juu ya kuongeza muda wa kukaa Stamford Bridge.

Santos ameiambia Tuttomercato; "Mkataba wake unaisha Juni 30, tuna pendekezo jipya kutoka kwa Chelsea na tutawapa kipaumbele."

Napoli pia wametajwa wanataka kumrejesha Jorginho kwa viongozi wa Serie A, na Santos alipendekeza kurejea kunawezekana iwapo mbinu itafanywa.



## HABARI MICHEZO

078,169/-

# SIMBA YATOA NENO USAJILI WA MIQUISSONE, MANZOKI


Luis Miquissone

Na Saada Akida

UONGOZI wa Simba umesema wanafurahi kuona wanahusishwa na usajili wa wachezaji Luis Miquissone na Cesar Manzoki katika kipindi hiki cha dirisha dogo na kuongeza watakapokamilisha mchakato huo watawatangazia mashabiki wao.

Miquissone anayekipiga katika klabu ya Al Ahly ya Misri ambayo inahitaji kumtoa kwa mkopo na Manzoki akiicheza DL Pro inayoshiriki Ligi Kuu ya China, wamehusishwa zaidi na Simba wakati dirisha dogo likiwa limefunguliwa.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wanafanya usajili mzuri na wanaenda kununua mikataba ya wachezaji wakubwa ambao wanawahitaji.

Alisema kuhusu Miquissone na Manzoki ni wachezaji wazuri na kulingana na uwezo wao hakuna timu isiyohitaji huduma za nyota hao ila wanaheshimu mikataba yao.

"Hao wachezaji wana mikataba na klabu zao, tunaheshimu sana na kama itakuwa wako katika mipango yetu basi tutalazimika kufanya nao mazungumzo na hizo klabu ila kwa sasa tunaheshimu mikataba yao," alisema Ahmed.

Aliongeza mapendekezo waliyopokea kutoka katika benchi la ufundi lililoko chini ya Juma Mgunda, watayafanyia kazi kwa kuwanasa wote wanaolengwa iwe kwa kutumia dau kubwa au kuvunja mikataba waliyokuwa nayo.

# SIMBA SC, YANGA DIMBANI

INATOKA UK. 32

mapema kwa ajili ya kufanya maandalizi lakini pia ratiba hiyo imezingatia uwepo wa michuano ya Kombe la FA (ASFC) inayoendelea na sababu nyingine za mikataba hasa kwa Azam TV.

"Febuari 12, na Mei 19 hadi 25 , itakuwa wiki ya Kombe la Shirikisho kwa raundi tano, kwa kuchezwa mzunguko wa 32, 16, robo na nusu fanali," alisema mtendaji huyo.

Alieleza bodi hiyo kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lilikaa pamoja na kukubaliana kupitisha mabadiliko ya ratiba ya ligi kwa lengo la kuakisi michuano iliyopo mbele kwa Stars, Simba na Yanga.

"Niwashukuru wadhamini tunaofanya nao kazi kwa mchango wao katika kutimiza yale matakwa ya kimkataba ambayo tumekubaliana, wadhamini watatu tuliokuwa nao ndio wanafanya timu zetu kusafiri na kufanya mambo mengine ya kifedha," Kasongo alisema.

Wakati huo huo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ametuma salamu zake za pole kufuatia kifo cha gwiji wa soka duniani Mbrazili, Edson Arantes do Nascimento maarufu kwa jina la Pele, kilichotokea juzi usiku.

"Mchango wake katika soka duniani utakumbukwa daima, pole kwa Rais wa Brazil @jairmessiasbolsonaro, familia na mashabiki wote wa soka. Mungu amweke mahali pema peponi, Amina," alisema Rais Samia.

Simba, Yanga, Azam FC na klabu nyingine za hapa nchini pia zimetoa salamu zao za pole kufuatia msiba huo.

"Rest In Peace Pele, Asante kwa furaha uliyoileta kwa mashabiki wa soka duniani," taarifa rasmi ya Yanga ilisomeka.

Taaifa mwili wa nyota huyo utaagwa rasmi keshokutwa na mazishi yake yatafanyika kwenye Makumbusho ya Necrópole Ecumênica, katika kaburi la wima huko Santos.

# YANGA, MTIBWA

INATOKA UK. 32

Yanga itashuka kwenye uwanja huo ikiwa na kumbukumbu ya kushinda mabao 2-0, yaliyofungwa na Fiston Mayele na Saido Ntibazonkiza ambaye hivi karibuni amejiunga na Simba.

Lakini katika mechi ya mzunguko wa kwanza msimu huu, Yanga ilishinda mabao 3-0, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, shukrani wafungaji ni Djuma, Fiston Mayele na Stephane Aziz Ki.

Yanga inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 47 wakati Mtibwa yenye pointi 24 iko kwenye nafasi ya nane.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 31/12/22 | 18:00 | AFC Bournemouth vs Crystal Palace | 2.80 | 3.20 | 2.48 |
| 02. 31/12/22 | 18:30 | Hapoel Tel Aviv FC vs Maccabi Netanya FC | 2.55 | 3.35 | 2.65 |
| 03. 31/12/22 | 18:30 | Sekhukhune United vs AmaZulu FC | 2.50 | 2.85 | 3.10 |
| 04. 31/12/22 | 19:00 | Bnei Sakhnin FC vs Hapoel Haifa FC | 2.49 | 3.20 | 2.80 |
| 05. 31/12/22 | 20:10 | FC Ashdod vs Hapoel Jerusalem FC | 2.65 | 3.20 | 2.65 |
| 06. 01/01/23 | 15:00 | Blackburn Rovers vs Cardiff City | 2.18 | 3.35 | 3.25 |
| 07. 01/01/23 | 17:00 | Angers SCO vs FC Lorient | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 08. 01/01/23 | 18:00 | Crewe Alexandra vs Tranmere Rovers FC | 2.75 | 3.20 | 2.55 |
| 09. 01/01/23 | 18:00 | Doncaster Rovers vs Carlisle United | 2.49 | 3.25 | 2.80 |
| 10. 01/01/23 | 18:00 | Hartlepool United vs Harrogate Town | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 11. 01/01/23 | 18:00 | Grimsby Town vs Stockport County FC | 3.05 | 3.25 | 2.31 |
| 12. 01/01/23 | 18:00 | Walsall FC vs Mansfield Town | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 13. 01/01/23 | 18:00 | Morecambe FC vs Burton Albion | 2.70 | 3.45 | 2.45 |
| 14. 01/01/23 | 18:00 | Blackpool vs Sunderland AFC | 2.85 | 3.15 | 2.49 |
| 15. 01/01/23 | 18:00 | Huddersfield Town vs Luton Town | 2.80 | 3.25 | 2.49 |
| 16. 01/01/23 | 18:00 | Colchester United vs Swindon Town | 2.95 | 3.20 | 2.36 |
| 17. 01/01/23 | 20:00 | Hapoel Hadera FC vs Maccabi Bney Reine | 2.40 | 3.15 | 3.00 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 31/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 2068 | Shahrdari Hamedan vs Kheybar Khorramabad FC | 4.19 | 2.63 | 2.08 |
| 13:30 | 2797 | Esteghlal Mollasani vs Saipa Karadj | 3.11 | 2.62 | 2.52 |
| 13:30 | 5167 | Peykan FC vs Sepahan Esfahan | 5.26 | 3.26 | 1.66 |
| 13:30 | 5201 | Sanat Mes Kerman FC vs Malavan Bandar Anzali | 2.18 | 2.67 | 3.74 |
| 14:00 | 5012 | Penafiel vs Viseu | 2.46 | 3.11 | 2.81 |
| 14:30 | 5238 | Nassaji Mazandaran vs Teraktor Sazi | 2.72 | 2.91 | 2.57 |
| 15:30 | 1409 | Wolverhampton vs Manchester Utd | 3.79 | 3.35 | 1.93 |
| 15:30 | 2205 | Abha vs Al Ittihad Jeddah | 4.60 | 3.65 | 1.73 |
| 15:30 | 2692 | AL Tai vs AL Baten | 1.23 | 5.63 | 13.06 |
| 15:30 | 5786 | Gol Gohar vs Persepolis FC | 3.21 | 2.77 | 2.34 |
| 15:55 | 4032 | AL Arabi vs Emirates Club | 2.83 | 3.56 | 2.15 |
| 16:00 | 2020 | Mtibwa Sugar vs Young Africans | 6.26 | 3.61 | 1.44 |
| 16:00 | 2365 | Young Sports Academy vs Astres FC de Douala | 2.49 | 2.90 | 3.10 |
| 16:00 | 3374 | Avion Academy vs Aigle Royal | 3.00 | 2.85 | 2.60 |
| 16:00 | 3844 | Barcelona vs Espanyol | 1.28 | 5.61 | 9.06 |
| 16:00 | 4083 | Beitar Jerusalem vs Sectzya Nes Ziona | 1.87 | 3.55 | 3.55 |
| 16:00 | 4382 | Albion Rovers vs Dumbarton | 3.26 | 3.26 | 2.05 |
| 16:00 | 5740 | Alloa Athletic vs Kelty Hearts FC | 1.99 | 3.45 | 3.40 |
| 16:30 | 2845 | Golden Arrows vs Kaizer Chiefs | 3.17 | 3.02 | 2.31 |
| 16:30 | 3077 | Richards Bay FC vs Moroka Swallows FC | 2.20 | 2.93 | 3.52 |
| 17:00 | 2813 | Dragon FC Yaounde vs Yafoot Yaounde | 3.00 | 2.85 | 2.60 |
| 17:00 | 3398 | Moreirense vs CF Estrela | 1.64 | 3.71 | 4.85 |
| 17:00 | 3452 | Renaissance de N. vs PWD Bamenda | 2.26 | 2.86 | 3.25 |
| 17:00 | 5534 | Union de Loum vs Feutcheu FC | 1.91 | 2.91 | 4.27 |
| 17:30 | 2640 | Flint Town United vs Gap Connahs Quay | 4.47 | 3.89 | 1.61 |
| 17:30 | 4795 | Haverfordwest vs Pontypridd Town | 1.65 | 3.85 | 4.29 |
| 17:30 | 5909 | Airbus UK Broughton vs The New Saints | 23.48 | 9.78 | 1.05 |
| 18:00 | 1215 | Ards FC vs Dundela FC | 2.26 | 3.73 | 2.57 |
| 18:00 | 2435 | Al Raed Club vs Al Taawon | 3.70 | 3.45 | 1.96 |
| 18:00 | 2843 | Newcastle vs Leeds | 1.43 | 4.57 | 6.16 |
| 18:00 | 3124 | Queen of South vs Clyde | 1.53 | 4.14 | 5.32 |
| 18:00 | 3366 | Manchester City vs Everton | 1.13 | 7.25 | 17.70 |
| 18:00 | 3555 | Bamboutos vs AS Fortuna | 1.72 | 3.35 | 5.20 |
| 18:00 | 4094 | Stirling vs Stenhousemuir | 1.85 | 3.75 | 3.41 |
| 18:00 | 4508 | Fulham vs Southampton | 1.95 | 3.51 | 3.56 |
| 18:00 | 4930 | Bournemouth vs Crystal Palace | 2.81 | 3.16 | 2.45 |
| 18:00 | 5733 | Sportive de Douala vs APEJES FC | 2.18 | 3.05 | 3.55 |
| 18:15 | 1801 | Villarreal vs Valencia | 1.94 | 3.41 | 3.81 |
| 18:15 | 5852 | Real Sociedad vs Osasuna | 1.86 | 3.35 | 4.29 |
| 18:30 | 2917 | Hapoel Tel Aviv vs Maccabi Netanya | 2.48 | 3.25 | 2.57 |
| 18:30 | 4825 | Sekhukhune United vs Amazulu | 2.44 | 2.82 | 3.17 |
| 19:00 | 1530 | Bnei Sakhnin vs Hapoel Haifa | 2.42 | 3.12 | 2.73 |
| 19:00 | 3866 | Azam vs Mbeya City | 1.48 | 3.55 | 5.87 |
| 19:30 | 3447 | Canon Sportif vs Colombe FC | 2.48 | 2.90 | 3.10 |
| 19:35 | 1860 | Al Ahli Jeddah vs AL Sahel SC | 1.63 | 3.85 | 5.00 |
| 20:10 | 4030 | FC Ashdod vs Hapoel Katamon | 2.57 | 3.10 | 2.57 |
| 20:30 | 1197 | Al Khaleej Club vs Al Nasr Riyadh | 14.00 | 5.80 | 1.21 |
| 20:30 | 2955 | Ironi Kiryat Shmona vs Maccabi Tel Aviv | 6.81 | 4.57 | 1.36 |
| 20:30 | 3234 | Al Hilal Riyadh vs Dhamk | 1.33 | 4.90 | 8.80 |
| 20:30 | 5170 | Brighton vs Arsenal | 3.23 | 3.28 | 2.15 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumamosi Desemba 31, 2022
Nipashe



## Brazil yatangaza siku 3 maombolezo ya Pele

UKURASA 29

MFALME PELE



Pele ambaye alijulikana kwa jina la "The King." akibebwa na mashabiki baada ya kuonyesha kiwango cha juu katika mechi ya fainali ya Kombe la Dunia iliyochezwa mwaka 1958 akiwa na Timu ya Taifa ya Brazil. Gwiji huyo aliweka rekodi ya kushinda mataji matatu ya Kombe la Dunia alifariki juzi akiwa na umri wa miaka 82. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA SC, YANGA DIMBANI APRILI 9

## •••Rais Samia aungana na wadau kumlilia Pele anayetarajiwa kuzikwa...

**Na Saada Akida**

SIMBA na Yanga zote zinatarajia kucheza mechi ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara ifikapo Aprili 9, mwakani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, imeelezwa.

Mchezo huo ulikuwa haujapangiwa siku kutokana na kalenda ya kimataifa iliyokuwapo awali kwa Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), Almasi Kasongo, alisema rasmi mchezo huo unaovutia mashabiki na wadau mbalimbali wa soka wa ndani na nje ya nchi, utachezwa kuanzia saa 11:00 jioni.

Kasongo alisema wamefanya mabadiliko kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ushiriki wa timu tano za Tanzania Bara katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yataanza kurindima kuanzia kesho Visiwani, Zanzibar.

"Kuna sababu saba ambazo tumeamua kufanya maboresho ya ratiba ya Ligi Kuu, ikiwamo Kombe la Mapinduzi, imekuwa ikiendelea kwa miaka mingi, tunatambua mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika michezo, tumeamua kufanya mabadiliko kwa sababu ya timu tano kutoka Bara kwenda kucheza michuano hiyo.

Sababu ya pili kuhusu timu yetu ya Taifa Stars kuhusiana na michuano ya CHAN, itakayofanyika nchini Algeria, katika ratiba yetu ya awali tuliweka timu yetu kufika mbali na kuipa nafasi lakini imeondolewa hivyo ratiba ikalazimika kufanyiwa maboresho," alisema Kasongo.

Ofisa huyo alitaja sababu nyingine ni michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika, kwa Yanga na Simba kwa kuwapa nafasi klabu hizo kujiandaa na michuano hiyo inayotarajiwa kuanza Februari.

"Wameondolewa mechi za karibuni ambazo wanatakiwa kucheza mwezi huo na kuwapa muda wa kujiandaa vizuri kuelekea michuano hiyo ya kimataifa kwa sababu ni wawakilishi pekee wa Tanzania.

Mabadiliko hayo pia yamezingatia Taifa Stars kuelekea michuano ya AFCON, tukiwa na mechi mbili, nyumbani na ugenini dhidi ya Uganda, mchezo huo utapigwa kati ya Machi 20 hadi 28, 2023," alisema Kasongo.

Aliongeza kuelekea michuano hiyo Taifa Stars inatakiwa kuingia kambini

INAENDELEA UK. 31

## Yanga, Mtibwa mechi ya hesabu

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi, Yanga watashuka kuwavaa wenyeji Mtibwa Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Manungu Complex, ulioko Turiani mkoani, Morogoro.

Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema katika mchezo huo watakosa huduma ya nyota wao mbalimbali akiwamo Khalid Aucho anayesumbuliwa na maumivu ya msuli huku Djuma Shaaban anaumwa malaria na Bernard Morrison amekwenda kwao Ghana baada ya kupata matatizo ya kifamilia.

Hata hivyo Morrison ameonekana katika mitandao akizindua taasisi yake binafsi tofauti na ilivyoelezwa.

"Wachezaji hawa waliopo Morogoro tunaamini wanatosha kabisa kuipambania Yanga, tunaimani kwa sababu tumecheza mechi ngumu nyingi ugenini na tumeshinda, kwa hiyo hata hii tutapata pointi tatu," alisema Kamwe.

Kocha wa makipa wa Yanga, Soud Slim, alisema wameajiandaa vyema kuelekea mechi hiyo licha ya kuwakosa wachezaji nyota.

"Ni mechi muhimu, ngumu na muhimu, utakuwa mchezo mzuri sana, tunacheza na timu ambayo mwaka huu imekuwa bora sana, ila tumejipanga kuitengeneza timu kwa ajili ya kupata ushindi. Na tumejiandaa kucheza kwenye hali zote, jua likiwaka au mvua ikinyesha," alisema kocha huyo na mchezaji wa zamani wa Mtibwa Sugar.

Wachezaji, Dickson Job na Kibwana Shomari ambao walijiunga na Yanga wakitokea timu hiyo walisema wanaiheshimu Mtibwa Sugar kwa sababu ni timu yao ya zamani na ni ngumu, hivyo wamejiandaa vilivyo kukabiliana.

"Sisi kama wachezaji tuko tayari, najua ni mchezon mgumu, Mtibwa ni timu nzuri, lakini naamini tutafanya vizuri," alisema Job.

"Mtibwa ni timu nzuri na ina wachezaji wazuri sana sisi kama Yanga tunaliheshimu hilo, ila kiu yetu kubwa kwenye mechi hiyo ni kupata pointi tatu," alisema Kibwana.

Yanga itajaribu kuendelea na wimbi lake la ushindi kwa mechi ya sita mfululizo, baada ya kupoteza kwa mara ya kwanza mabao 2-1 dhidi ya Ihefu Novemba 29, mwaka huu huku Mtibwa ikitoka kuchezea kichapo cha magoli 3-1 kutoka kwa Ihefu Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Highland Estates ulioko Mbarali, Mbeya.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042